# Nipashe

Alhamisi Julai 30, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580297

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Hatima ya uamuzi wajumbe wagombea CCM Agosti 8

UKURASA 4




UKURASA 11

# KWAHERI

• **Mkapa** azikwa rasmi, wananchi watembea Masasi hadi Lupaso, Kikwete asema ndiye aliyeasisi uchumi wa kati... *Endelea Ukurasa 2,4*



Mabrigedia Jenerali wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), wakishusha jeneza lenye mwili wa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Marehemu Benjamin William Mkapa katika mazishi yaliyofanyika Kijiji cha Lupaso, wilayani Masasi, mkoani Mtwara jana. **PICHA: IKULU**





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Vatican yaeleza kushtushwa na taarifa za kifo chake

UKURASA 3


**MICHEZO** **PLUIJM AAHIDI MAZURI YANGA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## JPM: Mkapa alitaka azikwe Lupaso

**Na Salome Kitomari,** MASASI

RAIS John Magufuli amesema Rais Benjamini Mkapa, alitaka kuzikwa kijijini kwake Lupaso wilayani Masasi na amehakikisha hilo linafanyika.

Vilevile, alisema umauti ukimfika, azikwe kijijini kwake Chato mkoani Geita na kwamba eneo lililotengwa Dodoma kwa ajili ya kuzikwa viongozi wa kitaifa ameligawa kwa wananchi na sehemu iliyobaki, itatumiwa na viongozi wanaotoka mkoa huo, akimtaja Waziri Mkuu mstaafu John Malecela.

"Kuna wakati serikali ilipanga sehemu ya maziko kwa viongozi na tulipangiwa kuzikwa Dodoma. Miaka miwili mitatu baadaye, Mzee Mkapa aliniuliza 'mlipanga maziko yawe Dodoma!' Mimi (Mkapa) msinizike Dodoma?'

"Nikamuuliza 'ungetaka kuzikwa wapi?', akaniambia nizikwe kijijini kwangu Lupaso. Nikamuuliza na Mzee Jakaya Kikwete (Rais wa awamu ya nne), akasema anataka azikwe Msoga mkoani Pwani.

"Sikumuuliza Mzee Ali Hassan Mwinyi kwa kuwa alikuwa na miaka 90 wakati huo, nikaona nikifanya hivyo nitakuwa namchuria. Nami kwa dhamira yangu nilisema kuzikwa nitazikwa Chato mkoani Geita. Hilo eneo atazikwa Malecela kwa sababu ni kwao, na kwa sababu hawatalitumia lote, nikawagawia wananchi. Utaratibu huu aliuanzisha yeye, Mkapa.

"Mkapa alipenda kwao, angeweza kuzikwa Dar es Salaam ambako ana eneo kubwa, ana mashamba mengi au Lushoto mkoani Tanga au angeweza kuzikwa kwingine kokote, lakini ndani ya dhamira yake alitaka kuzikwa sehemu yake alikozaliwa.

"Ninawapongeza wananchi kwa sababu katika kijiji hiki (Lupaso) alizaliwa mtu mzalendo na aliyependa watu wake na kwenye hili (upendo) ametuachia funzo kubwa sana," alisisitiza.

Taratibu za kuzika mwili wa Mkapa zilianza saa 8:30 mchana kwa taratibu za kijeshi zilizoambatana na wimbo maalum pamoja na wimbo wa taifa ulioimbwa na waombolezaji wote.

Taratibu za kijeshi zilikamilika saa 8:55 mchana, na Askofu Mkuu wa Jimbo la Tunduru Masasi, Filbert Mhasi, alilibariki kaburi na jeneza lenye mwili wa Mkapa lilishushwa kaburini na kikundi cha mabrigedia jenerali majira ya saa 9:04 alasiri kisha kaburi likaanikwa ardhini saa 15:10 alasiri.

Rais Magufuli, Mama Anna Mkapa na watoto wa Mkapa, waliongoza uwekaji wa udongo kaburini wakifuatwa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, Rais wa Zanzibar, Dk. Mohamed Ali Shein, Balozi Seif Ali Idd, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Marais Wastaafu Ali Hassan Mwinyi, Jakaya Kikwete, Spika Job Ndugai na Spika wa Baraza la Wawakilishi, Jaji Mkuu wa Tanzania na Jaji Mkuu wa Zanzibar, na Mwakilishi wa Mawaziri, Dk. Hussein Mwinyi, Mkuu wa Majeshi nchini na Rais wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Askofu Gervas Nyaisonga.

Kaburi lilifunikwa kwa mifuniko maalum yenye marumaru juu saa 15:25 alasiri kisha kuwekwa mashada na baadaye mazishi kukamilishwa kwa kupigwa mizinga 21.



Rais Dk. John Magufuli akishuhudia Mjane wa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Marehemu Benjamin William Mkapa, Mama Anna Mkapa, akiweka udongo kwenye kaburi la mume wake, katika mazishi yaliyofanyika Kijiji cha Lupaso, wilayani Masasi, mkoani Mtwara jana. **PICHA: IKULU**

# JK: Mkapa ndiye mwasisi Tanzania uchumi wa kati

**Na Mwandishi Wetu,** MASASI

RAIS mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, ameeleza upekee wa Rais mstaafu wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, huku akikumbusha kuwa ndiye mwasisi wa harakati za Tanzania kuwa nchi yenye uchumi wa kati.

Katika maziko ya mwili wa Mkapa yaliyofanyika jana Kijiji cha Lupaso wilayani hapa, Rais John Magufuli aliyekuwa anayaongoza, alitoa nafasi kwa marais wastaafu Kikwete na Ali Hassan Mwinyi kutoa salamu.

Baada ya kupewa fursa hiyo, Kikwete alitaja mambo mawili anayoyakumbuka kwa Mkapa, huku akikumbusha pia ushindani wao katika kumsaka mgombea urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1995.

Kikwete alikumbusha namna uongozi wa Mkapa ulivyoibua dira ya kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye uchumi wa kati, dira ambayo imekuwa ikitekelezwa na marais wote waliofuata kupitia mipango mbalimbali ya maendeleo, hasa ile ya miaka mitano mitano.

Juni 1999, Tanzania ilizindua Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, ambayo pamoja na mambo mengine, inalenga kupunguza nusu ya watu wanaoishi katika umaskini na kuwafanya wawe katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

"Ndiye alitengeneza dira ya 2025 kwamba wakati huu ukifika Tanzania iwe nchi ya uchumi wa kati na pato la mtanzania wa chini liwe dola 3,000. Nilipoingia, niliendelea nayo, na Magufuli ameendelea nayo, tumefika uchumi wa kati, lakini hatujafika kwenye alililotaka Mkapa, bado Dola 2,920, tukijipanga tunafikia.

"Mimi nilitengeneza mpango wa muda mrefu 2025 na kuugawa katika miaka mitano. Awamu ya kwanza ya mpango ni kuibua fursa za maendeleo Tanzania, na wa pili ni viwanda, wa tatu kuanzia 2021 hadi 2025 kuimarisha uwezo wa Tanzania kushindana katika soko la ukanda na dunia kwa ujumla," alisema.

Kikwete alisema kuwa Mkapa alibuni mipango mbalimbali ukiwamo Mpango wa Maendeleo ya Taifa (TASAF), huku akikiri kuwa alichukua nchi ikiwa katika hali ngumu kiuchumi, lakini alisimamia kwa nguvu zake zote licha ya maneno mengi na manufaa yalionekana baadaye kwa kuwa uchumi ulianza kukua kwa asilimia saba kwa mwaka.

"Tunamzika mtu aliyeyafanyia Tanzania mambo mazuri, hakumaliza yote, amefanya kwa wakati wake, ameliza safari yake kwenye urais, amefanya mengi makubwa ndani na nje, ameacha jina la Tanzania likiwa na sifa nzuri kwa kuwa amefanya mazuri kwa maslahi yetu, yaliyobakia ya viongozi wanaofuata," alisema.

Mbali na suala hilo la kiuchumi, Kikwete alisema mchakato wa uchaguzi mkuu wa mwaka 1995 ulionyesha Mkapa ni mtu wa kipekee kwa kuwa licha ya kuwa mpinzani wake mkuu ndani ya chama wakati wa mchakato wa kumsaka mgombea urais, kinyume cha matarajio yake, alimteua kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, jambo ambalo alilielezea kuwa 'ni nadra sana kwa siasa za Tanzania'.

"Tuligombea naye, mara ya kwanza nilishinda, lakini kura ziliporudiwa alishinda Mkapa na aliniteuwa kuwa waziri kwa miaka 10 mfululizo. Na kwa hali ya siasa zetu za Tanzania kwa uliyeshindana naye, dawa yake ni kumficha asionekane kabisaa, lakini yeye alinipa nafasi," alisema.

Kikwete alisema wakati wa uongozi wake, Mkapa alimsaidia kwa kiwango kikubwa na hakusubiri aitwe, bali alipiga simu kumwambia anataka kuonana naye.

"Kuna nyakati ngumu nilipita, nyakati ngumu na nzito sana, lakini Mzee Mkapa alikuwa ni moja ya nguzo zangu za kuegemea katika kile kipindi, alikuwa kiongozi mzuri na mwenye mapenzi makubwa kwa wananchi wa Tanzania, na alichukia mazingira ya umaskini," alisema.

Kikwete alisema alimfahamu Mkapa akiwa mwanafunzi, kipindi hicho Rais huyo wa awamu ya tatu akiwa mhariri na kwa mara ya kwanza alifanya kazi na kuishi naye kwa karibu alipokuwa Katibu wa CCM Wilaya ya Masasi, Mkapa akiwa Mbunge wa Nanyumbu.

Alisema mara baada ya Dk. Ali Hassan Mwinyi, kumteua kuwa Mbunge na Naibu Waziri wa Nishati na Madini akiwa Katibu wa CCM Masasi, alitumia maarifa ya Mkapa kuendesha jimbo.

"Jambo la pili, Mkapa alikuwa kiongozi thabiti mwenye utambuzi wa jambo lenye manufaa kwa watu wake. Nilipohamia hapa, nilimkuta marehemu Jaka Mwambi, wilaya ilikuwa inakabiliwa na ukame, kulikuwa na njaa, maji tabu, mimi na Mwambi tulibuni kilimo cha muhogo ambacho hakikupendeza sana kutokana na wazawa kutopenda ugali, lakini wakibanwa na njaa wanakula," alisimulia.

"Wapo waliopokea vizuri na wengine vibaya, wananchi wanaonung'unika, mbunge anayependa kusifiwa tu, angeweza kulalamika, barua ziliandikwa nyingi, lakini mbunge (Mkapa) alisimama thabiti na sisi na Masasi ikawa ya mfano ya mnachoweza kufanya mkikabiliwa na matatizo. "Hakujali kusifiwa maana unaweza kusifiwa ili uharibu, na hili limekuwa kwenye maisha yangu, nilimfurahia kwa uwezo wa kujenga hoja, kuwa na mawazo mazuri.

Kwa upande wake, Rais Mwinyi alisema nafsi yake imeghubikwa na huzuni, huku akirejea vitabu vitakatifu kuwa mwanadamu kwa maumbile yake ni mkosaji na kwamba Mkapa ni mwanadamu kama alivyo wengine na huenda katika umri wake amewahi kukosa.

"Katika hali kama hii, akiondoka ni kumwombea msamaha kwa Mungu endapo kama kakosea. Kama ana kosa, Mwenyezi Mungu amsamehe," alisema.

HABARI KITAIFA

# Vatican yaeleza ilivyopokea taarifa za kifo kwa mshtuko

**Na Salome Kitomari,** MASASI

VIONGOZI wa kitaifa na kimataifa wamemzungumzia Rais Benjamin Mkapa, huku Baba Mtakatifu wa Kanisa Katoliki duniani, Papa Fransis, akituma salamu za rambirambi kwa familia na Watanzania kufuatia kifo cha kiongozi huyo.

Katika salamu zake, Papa amesema Mkapa (1938-2020), alijitoa kuleta maendeleo kwa watu wake.

Salamu hizo za Papa na viongozi wengine wa kimataifa zilitolewa jana wakati wa misa ya maziko iliyofanyika majira ya saa nane mchana nyumbani alikozaliwa kiongozi huyo, Kijiji cha Lupaso, Kata ya Lupaso wilayani Masasi mkoani Mtwara.

Akiwasilisha salamu hizo, Rais wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Mhashamu Askofu Gervas Nyaisonga, alisema kwa kutambua kwamba Vatican, Rome ni nchi, Papa ametuma salamu kwa Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli.

Askofu Nyaisonga alinukuu ujumbe maalum wa Papa akisema: "Baba Mtakatifu amepokea kwa masikitiko sana (kifo cha Mkapa), anatoa salamu za rambirambi kwa familia na wote wanaoomboleza.

"Tunakumbuka miaka ya utumishi kwa kuendeleza elimu na kuleta maendeleo kwa watu wake. Baba Mtakatifu ameipendekeza roho ya marehemu Benjamini Mkapa kwa Mungu."

Salamu za Rais wa Msumbuji, Filipe Nyusi na Rais Mstaafu wa Msumbuji, Joaquim Chisano, zilisomwa na Balozi wa Msumbuji nchini, Monica Patrisio Mussa, akisema wanawatakia familia mshikamano na anatumaini wana nguvu ya kushinda wakati wa huzuni ya kifo cha mpendwa wao.

"Rais angependa kuwapo, lakini ameshindwa na ndiyo maana ametuma ujumbe, na ndugu yake Rais mstaafu Chisano, ametuma ujumbe wakati wa kumuaga ndugu na rafiki yake," alisema balozi huyo.

## Aliyesomeshwa na Mkapa hadi chuo kikuu afunguka

**Salome Kitomari na Hassan Nasri,** MASASI

SUNDAY Abdul, mmoja wa wananchi aliyesomeshwa na Rais mstaafu wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa, Sanday Abdul, ameeleza alivyoweza kufikia elimu yake kufika chuo kikuu kwa kusomeshwa na Rais Benjamin Mkapa, akilipiwa gharama zote za masomo.

Akizungumza na Nipashe wakati wa Maziko ya kiongozi huyo aliyefariki usiku a kuamkia Julai 24, mwaka huu, alisema walikuwa wanafunzi 12 waliofahulu katika shule msingi Lupaso ambako Mkapa alisoma na kuahidi kuwasomesha hadi atakaposhindwa wao.

Abdul alisema alimaliza Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), mwaka 2015 na kupata Shahada ya Ualimu na kwamba kwangu ni baba, kiongozi na mlezi kwa kuwa bila yeyea asingeweza kusoma.

Alikuwa anapenda elimu, aliniambia utasoma hadi pale utakapoacha kusoma, tulimaliza wote hatukumwangusha na wote tunafanya kazi sehemu mbalimbali. Pia kamsomesha mdogo wake.

Alisema alipata taarifa za msiba ikiwa ni siku chache akiwa ametoa kijijini, mdogo wangu aliingia mtandaoni na kunieleza Mzee amefariki nikahakikisha kwa kuingia mtandaoni niliona kwenye vyombo vya habari, nilikuwa Dar es Salaam naelekea Moshi ninapoishi, ikabidi nigeuze nirudi.

Alisema watu walimtegea sana na kwa sasa wanaona mambo mengi yatakwama kwa kuwa alikua na miradi mingi ikiwamo kuanzisha chuo cha Nesi, na kuimba serikali kusaidia miradi hiyo ikamilike.

Naye, Mwenyekiti wa Umoja wa Wanafunzi waliosoma Shule ya Sekobdari Ndanda, Godfrey Kasawala. ambako Hayati Mkapa alisoma, alisema kupitia umoja wao wamehuzunika kwa kuwa wamepoteza mwanachama na mlezi na kila mwaka huwa wana vikao vya kujadili maendeleo ya kuinua kiwango cha shule hiyo na kiongozi huyo alihudhuria.

"Septemba mwaka jana tulikaa kikao ambacho kilizaa matunda na serikali ilitoa miloni 674 kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa majengo mbalimbali," alisema




HABARI KITAIFA




Maofisa wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) wakiwa wamebeba jeneza lenye mwili wa Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu, Marehemu Benjamin William Mkapa, kuelekea eneo la makaburi kwa ajili ya mazishi, kijijini Lupaso, jana. **PICHA: IKULU**

# Maelfu wamzika Mkapa Lupaso

**Na Waandishi Wetu, MASASI**

KIJIJI cha Lupaso, Kata ya Lupaso wilayani Masasi mkoani Mtwara, jana kilizizima kutokana na wingi wa watu waliojitokeza kushiriki maziko ya Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamini Mkapa.

Maelfu ya wananchi walijitokeza katika kijiji hicho jana bila kujali jua, vumbi na umbali kutoka maeneo yao kwenda kuaga mwili wa kiongozi huyo.

Mwili wa kiongozi huyo uliwasili juzi alasiri ukitokea Dar es Salaam baada ya mazishi ya kitaifa, na kupelekwa moja kwa moja katika Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu Theresia wa Mtoto wa Yesu, Jimbo la Tunduru Masasi, ambako Mkapa alibatizwa na kutumikia katika maisha yake.

Baada ya misa, mwili ulipelekwa nyumbani na wananchi waliokuwapo waliaga, na ulilala nyumbani hadi jana asubuhi zilipoanza taratibu za maziko.

Misa ya maziko ilianza saa 2:14 asubuhi na kumalizika saa 9:52, ikiongozwa na Rais wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Mhashamu Askofu Gervas Nyaisongo.

**MAISHA YA HAKI**

Katika misa hiyo, Rais wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC), Askofu Nyaisongo, aliwataka watu kuishi maisha ya haki na uadilifu ili kusudio la Mungu lipate kutimia.

Alisema binadamu wote wanapaswa kutambua kwamba walipo ni wasafiri na wanapaswa kuishi na kutenda mema na kwa busara.

"Tuyajaze maisha yetu na fadhila mbalimbali ili yawe na maana mbele ya Mungu na wenzetu, tuwe na huruma, ukarimu, wema na usafi kama viungo vya Kristo, tutakutana naye kwa kusaidia maskini, wafungwa wagonjwa, wenye njaa, wafiwa na wanaoomboleza," alisema.

Askofu Nyaisongo alisema Rais Mkapa kila alipokwenda kusoma ndani na nje ya nchi, alijiunga na Chama cha Wanafunzi Wakatoliki, jambo ambalo ni fundisho kwa watu na kwamba hakuogopwa na watu ndani na nje ya kanisa, na hakuogopwa na watu wake aliowatumikia.

Alisema Rais Mkapa aliamini usawa wa binadamu wote na aliamini katika kutumikia wote kwa kutunza fadhila za uongozi, akisisitiza kuishi maisha ya kikristo, fadhila, imani, matumaini, upendo, sala, haki, unyenyekevu na toba.

"Kama mnavyoona, alifanya toba ya hadhara na kuandika kitabu chake cha 'My Life, My Purpose'. Toba hujenga, uvumilivu, msamaha, kujikatalia, uwajibikaji na nyingine nyingi ambazo zimebaki kama kielelezo cha kufikia uzima wa milele.

"Tunapotafakari juu ya kifo, lengo ni kutafakari juu ya uzima na maana ya maisha tuliyopewa na Mungu kama zawadi. Thamani ya maisha ya binadamu inatokana na kuyaishia maisha kwa ajili ya Mungu na kwa wenzetu," alisema.

Baada ya misa hiyo, viongozi na wananchi waliruhusiwa kutoa heshima za mwisho kwa mwili wa Mkapa, utaratibu ulioanza na maskofu wakuu, maskofu, mapadri, watawa na viongozi wa dini na baadaye waombolezaji wote.

Wananchi katika misururu mirefu waliaga mwili wa kiongozi huyo, huku wengine wakilia na kusema aliifungua kusini kimaendeleo kwa huduma za jamii kama hospitali, shule, maji na barabara.

**WANANCHI WATEMBEA**

Majira ya saa 12 alfajiri, wananchi wengi walikusanyika eneo la Bomani mjini Masasi, wakisubiri magari maalum yaliyowabeba kwenda Lupaso, huku wengine wakilazimika kutembea.

"Ninatamani ningeruhusiwa kutumia pikipiki yangu, ningeenda, ni lazima nikamzike huyu mzee, alikuwa alama yetu wana Masasi, lakini hapa lazima nisubiri utaratibu wa magari maalum yanayotupeleka," alisema Hamis Juma.

"Unaona tuna barabara ya lami kutoka mjini Masasi hadi kijijini kabisa, bila yeye tusingepata huduma hizi. Tunaomba Rais John Magufuli asitusahau, aendeleze maendeleo haya tusijisikie wapweke," alisema Abdalah Khamis.

■**Imeandikwa na Salome Kitomari na Hamis Nasir (MASASI).**


**REG.NA.: S.469**

**TANGAZO LA NAFASI ZA MASOMO KIDATO CHA TANO (V) KWA MICHEPUO YA HGL,HKL NA HGK**

Uongozi wa shule ya Sekondari Ivumwe unatangaza nafasi za kidato cha tano . Pia nafasi za kuhamia kidato cha kwanza na cha tatu.

KITAALUMA MWAKA 2018 (kimkoa ilikuwa ya 1 kati ya shule 36, na kitaifa ya 33 kati ya 543)

KITAALUMA MWAKA 2019 (kimkoa ilikuwa ya 2 kati ya 36,na kitaifa ya 60 kati ya 594).

***NAFASI HIZO ZIPO TANGU TAREHE 29/06/2020 MPAKA 15/08/2020.***

SHULE YA IVUMWE SEKONDARI IPO MKOANI MBEYA, ENEO LA IVUMWE KM 3 KUTOKA BARABARA KUU YA TUNDUMA HIGHWAY, PIA KARIBU NA CHUO CHA TEKU.

**MAWASILIANO: MKUU WA SHULE - 0754370878**
**TOVUTI :www.ivumwehighschool.sc.tz**
**WAHI SASA NA KARIBUNI SANA**

215833502


# Hatima uamuzi wa 'wajumbe' yanukia

**Na Elizabeth Zaya**

MWANGA wa kuwapata wabunge wa Viti Maalum kupitia Umoja wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), unatarajiwa kuonekana Agosti 8-10, vikao vya juu vya umoja huo vitakapoketi kupitia uamuzi uliofanywa na wajumbe waliowachagua.

Leo, wajumbe wanatarajiwa kuchagua wabunge kupitia umoja huo baada ya Umoja wa Wanawake wa chama hicho (UWT) kukamilisha uchaguzi wao Julai 23, mwaka huu.

Mchakato wa upigaji kura za maoni ulisimama kwa baadhi ya vyama vya siasa ikiwamo CCM, baada ya kifo cha Rais wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa aliyezikwa jana wilayani Masasi mkoani Mtwara.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa, Oganaizesheni ya CCM, Pereira Silima, alisema vijana hao watapigiwa kura na mabaraza ya chama hicho ya mikoa husika.

Silima alisema baada ya uchaguzi huo wa vijana, utakaofuata ni wa wazazi utakaofanyika Agosti Mosi ambao watapigiwa kura na jumuiya za wazazi za mikoa husika.

Silima alisema baada ya hapo, Agosti 8 hadi 10 itakuwa ni mchujo wa wagombea wa jumuia zote waliopitishwa kila mkoa.

"Na wagombea wote walioshinda katika jumuiya hizo, watapigiwa kura ya pamoja na Baraza Kuu la kila jumuiya na watakaoshinda ndiyo watakuwa wagombea na watachukuliwa mmoja kila mkoa"alisema Silima.

"Mtu ambaye atakuwa amekiuka maadili na mambo mengine, atashughulikiwa kwa sababu katika mchakato huu vinaangaliwa vigezo vingi ikiwamo kura alizopata, sifa zake kichama na kijamii na mambo mengine," alisema.

Silima alisema baada ya mchakato huo kumalizika, majina ya washindi yatapelekwa kujadiliwa kwenye vikao vya juu zaidi mkoani Dodoma.

# TANGAZO

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
*benki kwa maendeleo yako*

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.06.2020
## (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka Mwaka wa sasa 30-Jun-20 | Robo Mwaka Mwaka uliopita 31-Mar-20 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 11,205 | 9,631 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 12,195 | 11,436 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 22,000 | 26,870 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 209 | 203 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 197 | 40 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 5 | 7 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 0 | 0 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 75,395 | 81,567 |
| 12 | Mali Nyingine | 12,686 | 11,347 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 20 | 20 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 21,060 | 22,115 |
| 16 | JUMLA YA MALI | 154,973 | 163,236 |
| B. | DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 756 | 1,420 |
| 18 | Amana za Wateja | 110,868 | 110,406 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 0 | 0 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 1 | 1 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 3,315 | 2,766 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazol | 535 | 617 |
| 27 | Dhima Nyingine | 21,032 | 22,134 |
| 28 | Madeni | 779 | 5,137 |
| 29 | JUMLA YA DHIMA | 137,286 | 142,483 |
| 30 | MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)* | 17,687 | 20,752 |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 10,984 | 10,984 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 3,173 | 2,790 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (3,704) | (378) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 7,233 | 7,356 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| 37 | JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA | 17,687 | 20,752 |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 312 | 463 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 19,623 | 18,256 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 9,996 | 9,327 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 73 | 73 |
| D. | BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 11.4% | 12.7% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 22.5% | 19.8% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 76.2% | 81.2% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 56.2% | 56.5% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 63.0% | 66.6% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -0.2% | 1.2% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -5.1% | -3.6% |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
## KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.06.2020
## (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka sasa 30-Jun-20 | Robo ya mwaka Linganishi 30-Jun-19 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Jun-19 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 5,835 | 7,246 | 12,385 | 14,205 |
| 2 Gharama za Riba | (2,026) | (1,295) | (3,709) | (2,478) |
| 3 **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **3,809** | **5,951** | **8,677** | **11,727** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (2,251) | (468) | (2,374) | (608) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **1,153** | **1,894** | **2,470** | **3,767** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 61 | 109 | 134 | 157 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 803 | 1,435 | 1,801 | 2,967 |
| 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 6.4 Mapato Mengine | 289 | 350 | 535 | 643 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(6,037)** | **(7,065)** | **(12,476)** | **(14,356)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (3,267) | (3,575) | (6,582) | (7,336) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 7.3 Gharama Nyingine | (2,769) | (3,490) | (5,894) | (7,020) |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(3,326)** | **313** | **(3,704)** | **530** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 0 | (159) | 0 | (159) |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(3,326)** | **154** | **(3,704)** | **371** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(3,326)** | **154** | **(3,704)** | **371** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 420 | 448 | 420 | 448 |
| 14 Mapato kwa Hisa | (303) | 18 | (337) | 43 |
| 15 **Idadi ya Matawi** | **18** | **18** | **18** | **18** |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -8.4% | 0% | -4.7% | 0% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -69.2% | 3% | -38.5% | 3% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 121.7% | 90% | 111.9% | 93% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 14.8% | 22% | 16.8% | 22% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
## KWA MWAKA ULIOISHIA 30.06.2020
## (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo Mwaka ya sasa 30-Jun-20 | Robo Mwaka iliyopita 31-Mar-20 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-20 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Jun-19 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | (3,326) | (378) | (3,704) | 530 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | 0 | 0 | 0 | 0 |
| - Hasara Katika Mali | 704 | 764 | 1,468 | 801 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 6,172 | 3,178 | 9,350 | (5,513) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | (0) | 0 | 0 | (5) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (203) | 1,355 | 1,152 | (6,705) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 2,170 | 1,500 | 3,670 | 3,945 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (3,942) | (6,990) | (10,932) | 6,865 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (1,338) | (351) | (1,688) | (2,827) |
| - Kodi Iliyolipwa | (1) | (416) | (416) | 144 |
| - Mengineyo (bainisha) | 1,691 | (196) | 1,496 | 379 |
| ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **1,927** | **(1,532)** | **396** | **(2,386)** |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (23) | (46) | (69) | (506) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 0 | (0) | 0 | 6 |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 | (0) | 0 |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | **(23)** | **(46)** | **(69)** | **(501)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | (2) | (0) | (2) | 0 |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo (bainisha) | (1,006) | (695) | (1,701) | 0 |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(1,007)** | **(695)** | **(1,703)** | **0** |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 897 | (2,273) | (1,376) | (2,887) |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 16,351 | 18,624 | 18,624 | 19,584 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **17,248** | **16,351** | **17,248** | **16,698** |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30.06.2020

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2020** | **10,984,416** | **2,431,917** | **4,687,639** | **3,286,944** | **-** | **21,390,916** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | (3,703,790) | 0 | 0 | (3,703,790) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (1,514,439) | 1,514,439 | 0 | (0) |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | - | 0 | - | - |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 30.06.2020** | **10,984,416** | **2,431,917** | **(530,589)** | **4,801,382** | **-** | **17,687,126** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2019** | **8,607,136** | **2,431,917** | **7,546,745** | **2,537,257** | **779,217** | **21,902,272** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 371,234 | 0 | 0 | 371,234 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (114,812) | 149,646 | 0 | 34,834 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | (31,841) | 0 | 31,841 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Salio la mwisho wa mwaka 30.06.2019** | **8,607,136** | **2,431,917** | **7,771,325** | **2,686,904** | **811,058** | **22,308,339** |

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30.06.2020**

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

**Jina na Cheo** **Saini** **Tarehe**

Juliana Swai
**(Kaimu Mtendaji Mkuu)**

Bertha Simon
**(Mkuu wa Fedha)**

Chemo Mutani
**(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)**

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

**Jina** **Saini** **Tarehe**

1. Ernest Massawe
2. Dr. Josephat Daniel Lotto

**Sasa unaweza kulipia malipo yote ya Serikali (GePG) na Kodi za TRA kupitia Akiba Mobile na Matawi yetu yote ambayo hayana foleni."**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Pumzika Mkapa mwanadiplomasia na msuluhishi

**SAFARI** yako ya mwisho hapa duniani umeimaliza Rais wetu mstaafu Benjamin Mkapa na kulazwa kwenye nyumba yako ya milele kijijini kwako Lupaso, wilayani Masasi, mkoani Mtwara kama mwenyewe ulivyoagiza wakati ukiwa hai.

Katika uhai wako umefanya mengi ya kukumbukwa na yameshaelezwa kwa undani tangu umauti ulipokufika na kutangazwa rasmi kifo chako na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, John Magufuli.

Umahiri wako katika masuala ya kidiplomasia ulikufanya uheshimike si nchini kwako tu bali hata mataifa mbalimbali barani Afrika na duniani.

Nchini Kenya watakukumbuka kwa kazi kubwa uliyoifanya ya usuluhishi baada ya mgogoro wa kisiasa mwaka 2007 wakati wa uchaguzi wa urais nchini humo.

Wakati wa usuluhishi wewe ulikuwa mtu muhimu sana kwa kuruhusu maoni ya wananchi wa Kenya na kuyafanya yawe wazi kupitia vyombo vya habari.

Rais mstaafu Mkapa utakumbukwa pia kwa kuwa mpatanishi nchini Burundi na kuiwezesha nchi hiyo kuingia kwenye mchakato wa mazungumzo maarufu kama Inter Burundi Dialogue (IBD), ambao wewe kama kiongozi uliwezesha Burundi kuingia katika uchaguzi wa kwanza wa kidemokrasia na kupita katika kipindi cha mpito kwa amani.

Unguli wako katika masuala ya kidemokrasia ulitokana na kuaminiwa na hayati Rais wa kwanza wa Tanzania, Julius Nyerere, ambaye alikuteua kuwa balozi wa nchi mbalimbali barani Afrika na duniani na kuiwakilisha nchi yako kwa umahiri.

Utendaji wako mzuri ulikuwezesha kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje tangu serikali ya awamu ya kwanza na hata kipindi cha awamu ya pili kilichoongozwa na Rais mstaafu Ali Hassan Mwinyi, aliendelea kukuamini katika nafasi hiyo, licha ya pia kuteuliwa katika wizara nyingine zikiwamo ya habari.

Unyenyekevu wako, uchapakazi wako na mtu usiyependa makuu ulikujengea umaarufu mkubwa na wakati kipindi cha awamu ya pili kikimalizika, jina lako ndilo lililoibuka kuwa mgombea urais kwa awamu ya tatu na hatimaye kuchaguliwa kwenye uchaguzi mkuu kuwa Rais wa awamu ya tatu.

Ni katika kipindi chako cha urais uliwezesha Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo ilivunjika mwaka 1977 kuirejesha tena mwaka 1999.

Katika kipindi chako cha miaka 10 ya urais, kuanzia 1995 hadi 2005, Tanzania ilianza kukua kiuchumi na ushirikiano wa kibiashara kati ya nchi tatu waanzilishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo ni Tanzania, Kenya na Uganda na baadaye kuingizwa nchi za Rwanda na Burundi.

Baada ya kustaafu uliendelea na shughuli mbalimbali za kuhakikisha amani na utulivu vinaendelea kuwapo barani Afrika na ulikuwa umejikita katika mazungumzo ya amani nchini Burundi.

Ulianzisha taasisi yako iliyojulikana kama Mkapa Foundation, ambayo imekuwa msaada mkubwa wa kuendeleza masuala mbalimbali yawe ya kitaaluma na kimaendeleo pia.

Kitabu chako cha 'My Life, My Purpose' umeelezea mengi ya maisha yako ulipoanzia hadi ulipofikia ni alama kubwa umewaachia si Watanzania pekee bali mataifa mengine pia. Kuna mengi ya kujifunza kutoka kwenye kitabu chako. Utakumbukwa daima kwa sera yako ya 'Ukweli na Uwazi'.

Mwenyezi Mungu akulaze mahali pema peponi baba yetu mpendwa William Mkapa. Bwana ametoa na Bwana ametwaa jina lake lihimidiwe. **Amina.**

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kuelekea dalili ya kuanza rasmi hospitali iliyojengwa miaka 40

**HOSPITALI** ya Rufani ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, inayojengwa mjini Musoma mkoani Mara, inatarajia kuwa kubwa na kuhudumia mikoa yote katika ukanda wa Ziwa Victoria.

Uongozi wa mkoa hadi sasa umeamua kuendeleza ujenzi wa hospitali hiyo na umeahidi utahakikisha itakuwa na miundombinu, vifaa tiba na wataalamu wa kutosha, katika utoaji huduma za kibingwa katika fani zote muhimu.

Hivi sasa, hospitali inatarajia kuanza kutoa huduma za awali mwezi ujao, ambazo ni za mama na mtoto pamoja na matibabu ya figo, huku ukamilishaji miundombinu mingine ukiendelea.

Kuanza kutoa huduma hizo kunaelezwa na mkuu wa mkoa huo, Adam Malima, wakati akipokea vifaa vya kisasa kwa ajili ya kitengo cha matibabu ya figo cha hospitali hiyo mwanzoni mwa wiki hii.

Sababu za kuanza huduma hizo kabla ya nyingine, inaelezwa kuwa mkakati wa mkoa ni kuboresha afya ya mama na mtoto, kwa lengo la kuendelea kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Awali, mipango waliojiwekea ilikuwa ni kufikia Julai mwaka huu ujenzi uwe umekamilika na kuanza kutoa huduma, lakini haikuwa hivyo na sasa itaanza kutoa huduma hizo mwezi ujao, huku ukamilishaji ukiendelea.

Historia ya ujenzi wa hospitali hiyo inaanzia miaka ya sabini wakati serikali ya awamu ya kwanza na sasa inatarajia kuanza kutoa huduma mwezi ujao, ndani ya serikali iliyopo.

Kuchelewa kukamilisha ujenzi wa hospitali hiyo kumechangiwa na mengi ambayo simulizi yake ni ndefu, lakini itoshe kusema kwamba, kukamilika kwake kutakuwa ni ukombozi kwa wakazi wa mkoa huo.

Hospitali hiyo inajengwa katika Kitongoji cha Kwangwa kilichopo Kusini mwa mji wa Musoma, ambao uko kando ya Ziwa Victoria, ikiwa ni makao makuu ya mkoa huo.

Ujenzi huo ulianza zaidi ya miaka 40 iliyopita, ili wakazi wa mkoa wa Mara na mikoa ya jirani wapate huduma bora za afya na kwa uhakika, safari hii serikali inataka kuhakikisha inakamilika haraka.

Mwishoni mwa mwaka jana ujenzi wa hospitali hiyo ulianza kwa kishindo baada ya Rais Dk. John Magufuli, kuidhinisha zaidi ya Sh. bilioni 15 na sasa imefikia hatua ya kutaka kuanza kutoa huduma za awali.

Kuwapo kwa taarifa kwamba, hospitali hiyo itaanza kutoa huduma za awali mwezi ujao, ni habari njema kwa wakazi wa mkoa huo wilaya za Rorya, Tarime, Butiama, Serengeti, Musoma Mjini, Musoma na Serengeti.

Wakazi wa mkoa huo wamelazimika kila mara kwenda kupata huduma kubwa za afya katika Hospitali ya Rufani Bugando, jijini Mwanza, lakini sasa kuna nuru miezi michache ijayo, wataondokana na adha hiyo.

Hayo yapo bayana kwamba kuna kuanza kutoa huduma za awali ni dalili tosha kwamba kuna maendeleo mazuri ya ujenzi wa hospitali hiyo, ambayo kama nilivyoeleza, ujenzi wake una historia ndefu.

Tayari mkuu huyo wa mkoa, ameshaweka wazi kwamba lengo la serikali kutoa mabilioni ya shilingi ni kwa ajili ya kukamilisha mradi wa ujenzi wa hospitali hiyo, ili kuhakikisha wakazi wa mkoa wa Mara na jirani wanapata huduma bora za afya na za uhakika.

Kutokana na lengo hilo, anamtaka mkandarasi anayetekeleza mradi huo afanye kazi usiku na mchana, ili kufanikisha kile ambacho kimekusudiwa na serikali hasa kuboresha afya za wakazi wa mkoa wa Mara.

Miongoni mwa vitu mkandarasi anatakiwa kuvikamilisha ni uwekaji wa umeme na barabara kwa kuwa ni muhimu, kuwapo hospitalini hapo ili walengwa ambao ni wananchi waweze kunufaika na uwekezaji mkubwa unaofanywa na serikali katika hospitali hiyo.

Ni sehemu ya utekelezaji kitaifa wa Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM), ulioasisiwa mwaka 2007 na kuanza kutumika mwaka mmoja baadaye, ambako Mara nayo haikuwa nyuma.

**TANGAZO**

Yetu Microfinance Bank PLC
"Creating Wealth Together, Pamoja Tunaweza"

# YETU MICROFINANCE BANK PLC

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2020.
Kiwango kwa Tzs.

| | | Robo Mwaka wa sasa 30/Juni/2020 TZS | Robo Mwaka Ulipitia 31-Mar-20 TZS |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 552,113,424 | 434,705,550 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 1,518,437,963 | 149,472,231 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | | |
| 4 | Salio katika Benki Nyinginezo na Taasisi za Fedha | 211,389,828 | 807,700,286 |
| 5 | Hundi na Miamala ya kushughulikiwa | | |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | | |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | | |
| 8 | Dhima za Wateja zilizokubalika | | |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki Nyingine | | |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | | |
| 11 | Mikopo Halisi iliyopo | 12,516,370,063 | 12,909,499,804 |
| 12 | Mali Nyingine | | 1,834,871,521 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 1327352646.63 | |
| 14 | Akaunti za udhamini | | 768412744.05 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,340,278,703 | 1,286,495,780 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | 1,278,305,575 18744248202 | **18,191,157,916** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | | |
| 18 | Amana za Wateja | 1,794,837,146 | 2,164,847,020 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | | |
| 20 | Amana Maalumu | 1,408,799,117 | 1,716,933,574 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | | |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | | |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | | |
| 24 | Dhima la Tozo kwa ajili ya usuluhishi baina ya Benki na Mteja | | |
| 25 | Miamala isiyoshughulikiwa baina ya Matawi | | |
| 26 | Mapato yalioingia ya kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa baadae | | |
| 27 | Dhima Nyingine | 275,826,071 | 275,826,071 |
| 28 | Madeni | 7,000,000,000 | 5,500,000,000 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **10,479,462,335** | **9,657,606,666** |
| 30 | **MALI/{DHIMA} HALISI** | **8,264,785,868** | **8,533,551,250** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 6,056,496,547 | 6,056,496,547 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | | |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | | |
| 34 | Faida/{Hasara} ya Kipindi Husika | 2,332,349,000 | 2,332,349,000 |
| 35 | Akaunti zingine za Mtaji | (193,752,679) | 75,012,703 |
| 36 | Stahiki ya wenye Hisa chache | 69,693,000 | 69,693,000 |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **8,264,785,868** | **8,533,551,250** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | | |
| 39 | Mikopo chechefu | 708,105,024 | 797,397,524 |
| 40 | Tengo Kwa ajili ya mikopo chechefu | 746,149,373 | 832,647,159 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | | |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | % | % |
| i | Uwiano wa Fedha za wanahisa na Jumla ya Mali | 44.09% | 46.91% |
| ii | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 5.34% | 5.80% |
| iii | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 414% | 354% |
| iv | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 67% | 71% |
| v | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 71% | 76% |
| vi | Ongezeko la Amana | 1% | 1% |
| vii | Ongezeko la Mali | 3% | 2.63% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2020.
Kiwango kwa Tzs.

| | | Robo Mwaka wa sasa 30-Jun-20 TZS | Robo Mwaka Ulipitia 31-Mar-20 TZS | Limbikizo Robo Mwaka wa sasa 30-Jun-20 TZS |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 782,333,894 | 1,042,411,489 | 1,824,745,383 |
| 2 | Gharama za Riba | 87,397,260 | 87,808,219 | 175,205,479 |
| **3** | **Mapato Halisi (1 kutoa 2)** | **694,936,634** | **954,603,270** | 1,649,539,903 |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | | 0.00 | |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika mikopo | 86,531,234 | 59,324,608 | 145,855,842 |
| **6** | **Mapato yasiyo ya Riba:** | **212,752,725** | **160,966,204** | **373,718,929** |
| | 6.1 Faida/(Hasara) zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | | | |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 171,516,567 | 118,982,225 | 290,498,791 |
| | 6.3 Gawio | | | |
| | 6.4 Mapato Mengine | 41,236,158 | 41,983,980 | 83,220,138 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **1,187,973,271** | **1,128,860,855** | **2,316,834,126** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 613,536,406 | 562,444,865 | 1,175,981,270 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 30,191,146 | 28979475.38 | 59,170,622 |
| | 7.3 Gharama nyingine | 574,436,866 | 537,436,514 | 1,111,873,380 |
| 8 | **Faida/(Hasara) ya Uendeshaji** | **(193,752,679)** | **75,012,703** | -118,739,976 |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | | | 0 |
| 10 | **Faida/(Hasara ) Halisi baada ya Kodi ya Mapato** | **(193,752,679)** | **75,012,703** | -118,739,976 |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa{bainisha} | | | |
| 12 | **Jumla ya Faida/{Hasara} iliyojumuishwa kwa Mwaka** | **(193,752,679)** | **75,012,703** | -118,739,976 |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 121 | 134 | 121 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | -16 | 6 | -16 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 3 | 3 | 3 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 7.4% | 10.50% | 7.4% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 11.5% | 15.80% | 11.5% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 131% | 98.60% | 131% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 7.4% | 10.50% | 7.4% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2020
Kiwango kwa Tzs

| | | Robo Mwaka wa sasa 30-Juni-2020 TZS | Robo Mwaka Liganishi 31-Mar-2020 TZS |
|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **(193,752,679)** | **75,012,703** |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | - | - |
| | - Faida/{Hasara} kwenye Mauzo ya Mali | | |
| | -Uchakavu wa Mali za Kudumu | **5,199,423** | **7,199,423** |
| | -Uchakavu wa Matengenezo Makubwa | - | - |
| | -Utumikaji wa Mtaji wa Misaada | | - |
| | -Uchakavu wa Mali Zisizoshikika | - | - |
| | | **(188,553,256)** | **82,212,126** |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Salio la Benki Kuu ya Tanzania | | - |
| | - Badiliko Halisi katika Mikopo | | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (507,518,874) | 189,764,598 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 370,009,874 | 22,360,783 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika salio la benki Nyingine na Taasisi za Fedha | | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | - | - |
| | | **(326,062,256)** | **294,337,507** |
| | - Kodi Iliyolipwa | - | - |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **(326,062,256)** | **294,337,507** |
| | | - | - |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (8,190,205) | 27,370,412 |
| | Mapato kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Mali Zisizoshikika | - | - |
| | Mengineyo Amana za kudumu | | - |
| | Mapato kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | | - |
| | ***Fedha Halisi Zilizotolewa*** | **(8,190,205)** | **27,370,412** |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | 1,309,245,491 | (1,000,000,000) |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni Ya Muda Mrefu | | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | | |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | (84,929,881) | (63,727,889) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | | - |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha* | **1,224,315,610** | **(1,063,727,889)** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | Ongezeko/ Punguzo Halisi katika Fedha taslimu na Mali zinazofanana na Fedha | **890,063,148** | **(742,019,970)** |
| | Fedha na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka | **1,391,878,068** | **2,133,898,037** |
| | Fedha na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka | **2,281,941,216** | **1,391,878,067** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2020
Kiwango kwa Tzs.

| Kiwango kwa Tzs.'(000)' | Mtaji wa Hisa | Mtaji mkuu wa kisheria | Mtaji wa kisheria | | Akaunti zingine za Mtaji | Tengo la ziada ya juma | Jumla Tzs |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Salio la wa mwaka 01/01/2019 | 6,056,497 | 130,555 | - | - | 69,693 | 1,511,458 | 7,768,203 |
| Rekebisho : | | | | | | - | - |
| Ongeza: Jumlisha/(Futa) kwa kipindi cha robo | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato mengine | | | | | - | | - |
| Mtaji mkuu wa kisheria | | (130,555) | | | | 130,555 | - |
| Tozo la Mali la mwaka jana | | | - | | | 433,776 | 433,776 |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya kodi ya mapato | - | - | - | - | - | 681,377 | 681,377 |
| Gawio lililolipwa | | | | | | (424,817) | (424,817) |
| **Salio kwa Mwaka 31.12.2019** | **6,056,497** | **-** | **-** | **-** | **69,693** | **2,332,349** | **8,458,539** |
| **Salio la mwaka 01.01.2020** | **6,056,497** | **-** | **-** | **-** | **69,693** | **2,332,349** | **8,458,539** |
| Rekebisho : | - | | | | | | - |
| Ongeza: Jumlisha/(Futa) kwa kipindi cha robo | - | - | | | - | - | - |
| Toa: Mapato mengine | - | | | | | | - |
| Mtaji wa kisheria | - | | - | - | | | - |
| | - | | | - | | | - |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya kodi ya mapato | - | | | | | (193,753) | (193,753) |
| Toa: Gawio lililotolewa | - | | | | | - | - |
| **Salio kwa mwaka 30.06.2020** | **6,056,497** | **-** | **-** | **-** | **69,693** | **2,138,596** | **8,264,786** |

### ADA NA GHARAMA ZA HUDUMA KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2020
AINA YA BIDHAA

| 1. AKAUNTI ZA AKIBA | | | 2. Mkopo | |
|---|---|---|---|---|
| Kima cha chini cha kufungua akaunti | 5000/= | | Mikopo ya biashara | 3% pm |
| Ada ya mwezi | BURE | | Mikopo ya kuboresha nyumba | 1.4% pm |
| Taarifa ya Akaunti | BURE | | Ada ya Mkopo | 2.50% |
| Kuuliza salio | BURE | | Bima ya mkopo | 2.00% |
| Kufunga akaunti | 5000/= | | Mikopo ya Jikimu | 2% pm |
| Gharama za kuendesha akaunti | 5000/= | | Agricultural Loan | 2.5% pm |
| Gharama za kuweka fedha | BURE | | Mikopo ya kulipia Bima ya afya | 2% pm |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| Imesainiwa na: | Cheo | Tarehe: |
|---|---|---|
| *Altemius Millinga* | *Mkurugenzi Mtendaji* | *29-Jul-20* |
| *Samwel Gikaro* | *Meneja wa Fedha* | *29-Jul-20* |
| *Angela Fanuel* | *Mkaguzi wa Ndani* | *29-Jul-20* |

| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **65,050** | **53,101** | **64,066** | **52,187** | **135,944** | **82,864** | **133,668** | **81,050** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (19,220) | (15,656) | (19,220) | (15,656) | (40,100) | (24,315) | (40,100) | (24,315) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **45,830** | **37,445** | **44,846** | **36,531** | **95,844** | **58,549** | **93,568** | **56,735** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa** | | | | | | | | |
| | **Faida/(Hasara) uthamanishaji Dhamana za Kuuzwa** | **(955)** | **(4)** | **(955)** | **(4)** | **(932)** | **(210)** | **(932)** | **(210)** |
| | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **44,875** | **37,441** | **43,891** | **36,527** | **94,912** | **58,339** | **92,636** | **56,525** |
| 12 | Idadi ya Waajiriwa | 3,445 | 3,462 | 3,445 | 3,462 | 3,445 | 3,462 | 3,445 | 3,462 |
| 13 | Mapato kwa Hisa | 90 | 73 | 90 | 73 | 187 | 113 | 187 | 113 |
| 14 | Idadi ya Matawi | 226 | 223 | 226 | 223 | 226 | 223 | 226 | 223 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2.6% | 2.4% | 2.6% | 2.3% | 2.7% | 1.9% | 2.8% | 1.9% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 18.0% | 16.9% | 17.4% | 16.5% | 18.9% | 13.2% | 18.4% | 12.9% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 52.7% | 57.2% | 53.2% | 57.7% | 52.3% | 58.7% | 52.9% | 59.2% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 11.0% | 11.0% | 11.0% | 11.0% | 11.0% | 10.9% | 11.1% | 11.1% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | GROUP | | BANK | | GROUP | | BANK | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Robo Mwaka ya sasa | Robo Mwaka iliyopita | Robo Mwaka ya sasa | Robo Mwaka iliyopita | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
| | 30.06.2020 | 31.03.2020 | 30.06.2020 | 31.03.2020 | 30.06.2020 | 30.06.2019 | 30.06.2020 | 30.06.2019 |
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 65,050 | 70,892 | 64,066 | 69,601 | 135,942 | 82,864 | 133,667 | 81,051 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | | | | - | |
| - Hasara Katika Mali | 13,351 | 10,668 | 12,858 | 10,176 | 24,019 | 14,751 | 23,034 | 15,734 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (118,465) | (114,124) | (117,147) | (112,803) | (232,589) | (28,877) | (229,950) | (31,077) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 714,973 | (97,250) | 713,555 | (98,682) | 617,723 | 622,601 | 614,873 | 618,995 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 18,012 | (3,254) | 19,615 | (8,138) | 14,758 | 6,734 | 11,477 | 144,558 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (78,827) | 25,951 | (78,853) | 32,729 | (52,876) | 24,963 | (46,124) | (106,226) |
| - Kodi Iliyolipwa | (43,090) | (19,021) | (43,090) | (19,021) | (62,111) | (26,357) | (62,111) | (26,357) |
| - Mengineyo (bainisha) | 19,407 | 12,630 | 19,407 | 12,630 | 32,037 | (34,375) | 32,037 | (34,375) |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **590,411** | **(113,508)** | **590,411** | **(113,508)** | **476,903** | **662,303** | **476,903** | **662,303** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (4,650) | (4,361) | (4,650) | (4,361) | (9,011) | (13,054) | (9,011) | (13,054) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | (38,003) | (168,983) | (38,003) | (168,983) | (206,986) | (183,887) | (206,986) | (183,887) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(42,653)** | **(173,344)** | **(42,653)** | **(173,344)** | **(215,997)** | **(196,941)** | **(215,997)** | **(196,941)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | (48,000) | - | (48,000) | - | (48,000) | (33,000) | (48,000) | (33,000) |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 54,271 | (26,274) | 54,271 | (26,274) | 27,997 | (27,799) | 27,997 | (27,799) |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **6,271** | **(26,274)** | **6,271** | **(26,274)** | **(20,003)** | **(60,799)** | **(20,003)** | **(60,799)** |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | | | | | |
| **Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **554,029** | **(313,126)** | **554,029** | **(313,126)** | **240,903** | **404,563** | **240,903** | **404,563** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 900,244 | 1,213,370 | 900,244 | 1,213,370 | 1,213,370 | 856,178 | 1,213,370 | 856,178 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **1,454,273** | **900,244** | **1,454,273** | **900,244** | **1,454,273** | **1,260,742** | **1,454,273** | **1,260,742** |

## TAARIFA YA KUNDI YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Uthamanishaji Amana za Kuuzwa) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | **-** | **944,472** | **-** | **-** | **4,630** | **969,102** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 95,844 | - | - | - | 95,844 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (931) | (931) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (48,000) | - | - | - | (48,000) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | **-** | **992,316** | **-** | **-** | **3,699** | **1,016,015** |
| **Mwaka Uliopita 2019** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | **-** | **799,128** | **-** | **33,725** | **4,342** | **857,195** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 58,550 | - | - | - | 58,550 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (882) | (882) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | (1,985) | - | (1,985) |
| Gawio lililolipwa | - | - | (33,000) | - | - | - | (33,000) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (994) | - | - | - | (994) |
| Mengineyo | - | - | 1,599 | - | - | - | 1,599 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | **-** | **824,963** | **-** | **35,710** | **3,460** | **884,133** |

## TAARIFA YA BENKI YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2020

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Uthamanishaji Amana za Kuuzwa) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | **-** | **951,341** | **-** | **-** | **1,049** | **972,390** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 93,568 | - | - | - | 93,568 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (932) | (932) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (48,000) | - | - | - | (48,000) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | **-** | **996,909** | **-** | **-** | **117** | **1,017,026** |
| **Mwaka Uliopita 2019** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **20,000** | **-** | **808,448** | **-** | **33,725** | **881** | **863,054** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 56,736 | - | - | - | 56,736 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (210) | (210) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | (33,000) | - | - | - | (33,000) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (1,314) | - | 1,314 | - | - |
| Mengineyo | - | - | (3,097) | - | - | - | (3,097) |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **20,000** | **-** | **827,773** | **-** | **35,039** | **671** | **883,483** |

## BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2020

**Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.**

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Ruth Zaipuna<br>**Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu** | | Julai 27, 2020 |
| Benedicto Baragomwa<br>**Kaimu Afisa Mkuu wa Fedha** | | Julai 27, 2020 |
| Juma Kimori<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | | Julai 27, 2020 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Dr. Edwin P. Mhede<br>**Mwenyekiti wa Bodi** | | Julai 27, 2020 |
| Leonard Mususa<br>**Mkurugenzi** | | Julai 27, 2020 |

www.nmbbank.co.tz

TANGAZO

# MINIMUM DISCLOSURE OF BANK CHARGES AND FEES

NMB
Karibu yako

| S/N | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE |
|---|---|---|
| 1 | SAVINGS ACCOUNTS | |
| | Required minimum opening balance | Business saving A/C TZS 100,000, USD 100,EUR 100,GBP 100; Bonus A/C TZS 50,000, USD 100, EUR 100 & GBP 100; Mtoto A/C TZS 7,000 or USD/EURO/GBP 5; Chipukizi A/C TZS 7,000 or USD/EURO/GBP 5; Pamoja A/C TZS 30,000 |
| | Transaction fee | N/A |
| | Monthly service fee ( break down per customer type) | FREE |
| | Statement | TZS 2000 per month |
| | Withdrawal Charges | OTC: TZS 4,000 for amount up to TZS 5Million; TZS 4,000plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/-; OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Withdrawal bulky without notice | OTC: TZS 4,000 for amount up to TZS 5Million; TZS 4,000plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/-; OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Cash Deposit Charge | 5% of the amount for small denomination FOREX (1,5,10 & 20) For LCY deposit of coins 10% of the amount |
| | Savings Card/Passbook | N/A |
| | Passbook/Card Replacement | TZS 11,800 |
| | Closing Account | TZS 9,440 USD 11.8, EUR 11.8 & GBP 11.8 |
| 2 | CURRENT ACCOUNT | |
| | Required minimum opening balance | Business, Supply Chain, Trade Business, Agribusiness Overdraft, Agribusiness Loans, Agri-General, Business AC Plus, Corporate, Emerging Corporate A/C - TZS 100,000, USD 100, EUR 100 & GBP 100; Personal A/C - TZS 15,000; Mwanachuo & Chapchap A/C - TZS 10,000; Wisdom - FREE; Group A/C - TZS 30,000; Fanikiwa A/C - TZS 20,000; Exclusive A/C - TZS 1Million; Executive A/C - TZS 500,000; Kilimo & Bonus A/C - TZS 50,000; Float & Scheme Financing A/C - FREE; Notice Investment A/C - TZS 500Million;Chapchap Plus (NMB Mkononi)- ZERO |
| | Monthly service fee ( break down per customer type) | Personal A/C - TZS 1,800; Business A/C - TZS 15,340; Agribusiness,Corporate, Insitution & Trade Business A/C - TZS 19,200; Exclusive A/C - TZS 35,400; Executive A/C - TZS 23,600; Emerging Corporate - TZS 19,200; Fanikiwa - TZS 2,000; Personal A/C Agribusiness - TZS 2,048; Kilimo is FREE; for Forex A/C charges are Equivalent to TZS;Chapchap Plus (NMB Mkononi)- FREE |
| | Transaction fee | N/A |
| | Statement | TZS 2000 per month |
| | Withdrawal Charges | OTC: TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/- ; OUR ATM - TZS 1,100 -1,500; OTHERS DOMESTIC ATM - TZS 3,540; OTHERS OUTSIDE TANZANIA - TZS 7,080; POS - TZS 1,770 |
| | Cash Deposit Charge | 5% of the amount for small denomination FOREX (1,5,10 & 20) For LCYdeposit of coins 10% of the amount. |
| | Bank Drafts | NA |
| | Bank Drafts cancellation charge | NA |
| | Cheque book (100 leaves) | TZS 48,380 USD 35.4, EUR 23.6 & GBP 17.7 |
| | Cash Withdrawal at Counter | TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/- |
| | Special Clearance | TZS 53,100 USD 52.8, EUR 46 & GBP 39.5 |
| | Cheque withdraw over the counter | TZS 6,500 for amount up to TZS 5Million; TZS 6,500plus 0.12% of excess above TZS 5Million Max TZS 170,000/- |
| | Dishonoured cheque | 1.5% of the amount Min 64,000 Max TZS 118,000 |
| | Cash Payment to 3rd party | N/A |
| | Cash Deposit Charge | N/A |
| | Overdrawn account interest charge | N/A |
| | Unarranged Overdraft | N/A |
| | Bulk cash Deposit | FREE |
| | Bulk cash Withdrawal | N/A |
| | Stop Payment orders | TZS 35,400, USD 23.6, EUR 17.7 & GBP 17.7 |
| | Standing Orders ( within the same bank) | FREE |
| | Standing Orders ( to other bank) | TZS 19,710 |
| | Letter of introduction | N/A |
| | Salary handling | TZS 3,540 |
| | School fees deposits | FREE |
| | TRA collection | FREE |
| | Safe custody charges | N/A |
| | Safe custody access fees | N/A |
| 3 | EFT | |
| (a) | Within the same bank (On Us) | FREE |
| | To other Banks ( On Others) | 2000 |
| (b) | Outward Transfers | 2000 |
| | Inward Transfers | FREE |
| 4 | TISS | |
| (a) | Within the same bank (On Us) | N/A |
| | To other Banks ( On Others) | TZS 10,000 |
| (b) | Outward Transfers | TZS 10,000 |
| | Inward Transfers | FREE |

| 5 | FOREIGN EXCHANGE ACCOUNT | Savings Acc | Current Acc |
|---|---|---|---|
| | Statement | USD 1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month | |
| | Interim statement | USD 1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month | USD1, EUR 0.8 and GBP 0.7 Per month |
| | Withdrawal Charges | 0.25% of the amount - forex | 0.25% of the amount - forex |
| | Cash Deposit Charge | 5% for small denomination (1,5,10 & 20) | 5% for small denomination (1,5,10 & 20) |
| | Purchase/Sale of TC transactions over the counter | N/A | N/A |
| | Purchase of Foreign Cheque | N/A | N/A |
| | Sale/ Purchase of cash passport | N/A | N/A |
| | Telex/SWIFT | USD 58 | USD 58 |
| | Transfer from foreign currency denominated account to local account | N/A | N/A |
| | Outward foreign transfers | USD 58 | USD 58 |
| | Inward foreign transfers - Customers | FREE | FREE |
| 6 | ATM TRANSACTIONS | | |
| (a) | Local Cards | | |
| | Issue of ATM card | N/A | N/A |
| | Replacement ATM Card (Faulty) | N/A | N/A |
| | Replacement ATM Card (Lost) | N/A | N/A |
| (b) | International Cards | | |
| | Issue of ATM card | N/A | Tanzanite - TZS 11,800; Titanium - FREE; World Reward - FREE |
| | Replacement ATM Card (Faulty) | N/A | Tanzanite - TZS 11,800; Titanium - TZS 23,600; World Reward - TZS 35,400 |
| | Replacement ATM Card (Lost) | N/A | Tanzanite - TZS 11,800; Titanium - TZS 23,600; World Reward - TZS 35,400 |
| (c) | ATM Withdrawals: | | |
| | Within the same bank (On Us) | N/A | From TZS 1,100 - 1,500 |
| | To other banks ATM (On others) | N/A | TZS 3,540 |
| | ATM mini statement | N/A | TZS 413 |
| | Bill payments through ATM | N/A | FREE |
| (d) | POS | | |
| | Within the same bank (On Us) | N/A | TZS 1,770 |
| | To other banks ATM (On others) | N/A | FREE |
| 7 | MOBILE (SMS) BANKING | | |
| | Balance Inquiry | N/A | TZS 360 |
| | Payments | N/A | FREE |
| | Transfers (within NMB) | N/A | FREE |
| 8 | INTERNET BANKING | | |
| (a) | Domestic: | | |
| | Balance Inquiry | FREE | FREE |
| | Payments | TZS 640 | TZS 640 |
| (b) | International | | |
| | Balance Inquiry | N/A | FREE |
| | Payments | N/A | FREE |
| | Transfers | N/A | USD 45 |
| 9 | MONEY REMITTANCES | | |
| (a) | Western Union | | |
| | Sending | N/A | N/A |
| | Received | N/A | N/A |
| (b) | Money Gram | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (c) | Coinstar | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (d) | Travelex | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (e) | Africash | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |
| (f) | Others (Specify) | | |
| | Inward | N/A | N/A |
| | Outward | N/A | N/A |

| 10 | BANKING SECTOR - DEPOSITS & LENDING RATES | | |
|---|---|---|---|
| A | TYPES OF LENDING RATES | LENDING RATES - PA (%) | |
| | | TZS | USD |
| (a) | Flat | | |
| (b) | Declining | 17% | 9% |
| (c) | Negotiable | | |

B FIXED DEPOSITS

| PERIOD | TZS | | | USD | GBP |
|---|---|---|---|---|---|
| | 500K><9.9Mil | 10M><99.9M | 100M><199M | 2000-49,999 | 2000-49,999 |
| I Month | 2.00% | 2.25% | 2.50% | 0.45% | 0.25% |
| 2 Months | 2.50% | 2.75% | 3.00% | 0.55% | 0.30% |
| 3 Months | 3.00% | 3.25% | 3.50% | 0.70% | 0.40% |
| 6 Months | 3.50% | 4.00% | 4.50% | 0.80% | 0.50% |
| 9 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |
| 12 Months | 5.00% | 6.00% | 7.00% | 1.00% | 0.60% |
| 13-24 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |
| 25-36 Months | N/A | N/A | N/A | N/A | N/A |

**Signed By:**

**Aloyse Maro**
**Head of Retail Products and Channels**

**Filbert Mponzi**
**Chief Retail Banking**



AFYA

# Hofu mashine ya ‘microwave’ kubebesha watumiaji maradhi

• WHO yaitetea, wataalamu wadai ‘shida ipo’
• Bakuli za plastiki nazo njia panda nyingine



Mashine ya ‘microwave’ katika matumizi tofauti. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

MASHINE aina ya ‘microwave’ imekuwa na manufaa makubwa katika suala la upishi na uhalisia wa matumizi yake umetapakaa kila mahali duniani, kwa mujibu wa teknolojia ya sasa.

Yapo mazoea kwamba kwa wasioweza kupika, wavivu au wasiotaka kupika, huichukulia katika sura ya mkombozi wa mapishi. Katika matumizi inachukuliwa kuwa na uwezo wa kumaliza jukumu la sanaa ya upishi.

Hata hivyo, kuna mjadala mwingine unaohusu mzozo uliopo kuhusu mashine inayopitia swali, ni wakati gani upishi kwa kifaa ‘microwave’ hauko salama kwa afya yako?

Shirika la Afya Duniani (WHO), lina matazamo wake kwamba hakuna la kutia shaka pale mionzi inayotumika kupasha moto chakula hicho, inapotumika vyema.

### VIRUTUBISHO KUHARIBIKA?

Kuna utafiti unaofanywa na kuonyesha kwamba mimea inapoteza thamani ya virutubisho vyake ndani ya mashine, lakini mtazamo katika hilo, ni kwamba ama kuongezeka au kupungua thamani ya virutubishi katika chakula, kunategemea muda wa upishi.

Hata hivyo, kunatajwa kuwapo utafiti mwingine wa mwaka jana, uliochunguza virutubishi katika mapishi ya ‘microwave’ ulibaini utafiti wa awali ulitofautiana kuhusu muda na kiwango cha joto ndani ya maji.

> **Kuna baadhi ya plastiki zimepigwa marufuku kuingizwa katika vifaa ‘microwave’ kwa sababu hazimudu kuingizwa katika chakula kwenye nyuzi joto zaidi ya 100.**

Ilibainika, kutumia mashine hiyo kwa dakika moja hakupunguzi virutubishi na upishi wa kutumia mvuke na ule wa ‘microwave’,bali unaweza kuongeza virutubishi ambavyo ni viungo vinavyohusishwa na kupunguza hatari ya ugonjwa wa moyo.

Kwa mujibu wa watafiti, inapozingatiwa kanuni za upishi wa ‘microwave’ ulisaidia kuhifadhi virutubishio, ila kuna angalizo kwamba, maji yanapozidishwa kwenye microwave, hupunguza viungo hivyo muhimu.

Xianli Wu, ni Mtafiti Mkuu na Mwanasayansi katika Idara ya Kilimo, katika Kituo cha Utafiti wa Virutubisho cha Beltsville, Marekani unasema kwamba makubaliano kuhusu mpango wa kuelezea upishi wa kutumia ‘microwave’ unaweza kuongeza viungo vinavyoboresha kinga za mwilini.

Pia, anasema kuna vyakula vinavyoongezewa na vingine haviongezewi, lakini hakuna jibu rahisi iwapo mboga hizo zitahifadhi virutubishi vingi katika nyenzo nyinginezo za mapishi.

Inaelezwa hiyo inatokana na ukweli kwamba kila chakula kina viwango vya virutubishi tofauti kulingana na mtazamo wa mtafiti Wu.

Anasema, ingawaje mashine hiyo inatumika katika sehemu nyingi, lakini namna inavyotumika ni tofauti kwa kila aina ya mboga.

### VYOMBO PLASTIKI

Inaelezwa, iwapo chakula kinachopikwa na kifaa ‘microwave’ kipo hatarini kupoteza virutubisho. Pia, kupasha chakula ndani ya chombo cha plastiki, nako kunatajwa kugusa afya ya umma.

Wanasayansi wana maono kwamba, kuna hatari ya kula kemikali hatari zinazotokana na vifaa vya plastiki, zinazoelezwa kuangukia hatari zinapokolea moto, kemikali za plastiki zinayeyuka na kuingia katika chakula.

Kuna baadhi ya plastiki zimepigwa marufuku kuingizwa katika vifaa ‘microwave’ kwa sababu hazimudu kuingizwa katika chakula kwenye nyuzi joto zaidi ya 100.

Mtaaluma, Profesa Juminga Tang, mtaalamu wa uhandisi chakula katika Chuo Kikuu cha Washington, nchini Marekani, anarejea utafiti uliofanywa mwaka 2011.

Anasema, watafiti walinunua zaidi ya vyombo 400 vya kuweka chakula vya plastiki na walibaini kwamba kemikali nyingi zinazopotea, hudhuru homoni mwilini mwa binadamu.

Watafiti wanasema kuna kemikali zinazoongezwa katika plastiki ili kuzifanya kujipinda hupatikana katika vyombo vya plastiki na chupa za maji.

Kemikali hizo zimebainika kuingilia homoni na mfumo wa chakula mwilini, kwani kemikali hizo huchangia magonjwa ya pumu na tatizo katika mfumo wa mimba kwa kinamama.

Vilevile kemikali kuna athari ya utendakazi wa homoni ambazo ni muhimu katika utengenezaji wa ubongo wa mtoto.

### ATHARI YA MVUKE

Wataalamu wana maoni kwamba, hata mpishi asiyependelea vyombo vya plastiki katika ‘microwave’ lakini bado kuna hatari kubwa ya kutumia vyakula vinavyopikwa na ‘microwave.’

Mtazamo mmoja unaangukia kwamba nguvu ya mvuke katika chakula haitapakai kote katika chakula kitakachopikwa,

Cha muhimu kinachoshairiwa anasema ni ‘microwave’ inapaswa kutumika kupasha chakula moto, badala ya kupikia. Sababu kuu ni kwamba, inapika upande mmoja wa kwingineko kunabaki.

Profesa Francisco Gonzalez, mtaalamu wa Usalama wa Chakula, katika Chuo Kikuu cha Georgia, Marekani, chakula kinapaswa mara moja katika microwave.

Vilevile, kupasha chakula moto kunatajwa hatari. yake inapopashwa moto wa nyuzi joto sentigdredi 82 kila mahali kuweza kuwaua bakteria hatari na inashauriwa haifai chakula kupasha zaidi ya mara moja.

### UPASHAJI WA ‘MICROWAVE’

Japo viwango vya joto sio tatizo, lakini kuna utafiti unataja hatari inayohusishwa na kutumia ‘microwave’ kwa vyakula vya jamii ya wanga kama vile nafaka, ikiwamo wali na uji, na vinavyokuzwa katika mizizi, kama vile mihogo.

Viwango vya juu vya joto katika ‘microwave’ husababisha kemikali kwa itawayo ‘acrylamides’ inayopatikana mara nyingi mtu anapopika viazi. Kuna madai kwamba inadhuru utendaji kazi wa chembe hai.

Hata hivyo, kuna ushahidi kama huo katika binadamu. Kuna utafiti unaosema kwamba ‘microwave’ husababisha kemikali hiyo zaidi ya mbinu nyingine yoyote ya kupikia.

“Katika kiwango cha nyuzi joto (sentigterdi) 100, kuna nguvu ya kutosha kubadilisha muundo wa moja kwa moja kati ya molekyuli ili kutoa ‘molekyuli’ yenye nguvu nyingi, inayoweza kuguswa na DNA (kinasaba)na kusababisha kuzaana,” anasema Profesa Schwartz.

Kemikali hiyo inahofiwa kuna hatari katika uzazi na ufaiti uliofanyika kwa wanyama, umeonyesha ni hali inayochangia kusababishwa na kemikali za ‘acrylamides.’

Njia moja ya kudhibiti hatari hiyo, ni kuzamisha viazi kwenye maji kabla ya kuziweka kwenye ‘microwave.’

Kuhusu hofu ya athari za mionzi kwenye chakula, wataalamu hao wamebaini kwamba bado ni salama na sababu kubwa ni kwamba, inatumia kiwango cha chini cha elektroniki ikifafanishwa na kile kwenye balbu na redio. **BBC**





# Bodi yataka hatua wataalamu wakiuka taaluma mipango miji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BODI ya Mipango Miji imeagizwa kuwafuatilia na kuwachukulia hatua wataalamu wanaokiuka maadili ya taaluma zao kwenye upangaji wa miji.

Agizo hilo lilitolewa jana jijini hapa na Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ezekiel Mpanda, alipokuwa akifungua kikao kazi cha kujadili utafiti kuhusu mipango miji uliofanywa na Chuo Kikuu cha Ardhi kwa maofisa wa mipango miji na watendaji wa wizara kwa niaba ya Naibu Katibu Mkuu, Nicolaus Mkapa.

Alisema bodi hiyo ina wajibu wa kuwafuatilia wataalamu wa mipango miji kuhakikisha wanafuata sheria, kanuni na taratibu za upangaji miji. "Bodi ifuatilie na kuwachukulia hatua wataalamu wa mipango miji wanaokiuka maadili ya kazi zao. Kwa muda mrefu sana sasa tumeshuhudia malalamiko kwenye maeneo mbalimbali nchini kuhusu kazi za mipango miji, hususan urasimishaji unaofanyika nchini," alisema.

Aidha, Mpanda alisema wataalamu wa mipango miji wameacha jukumu lao la kupanga miji na kuziachia kampuni binafsi bila usimamizi madhubuti hali iliyosababisha kampuni hizo kuchukua fedha nyingi za wananchi na kutofanya kazi.

"Yako (ziko) makampuni (kampuni) yenye (zenye) tabia hii nchini ikiwamo Jiji la Dar es Salaam na Arusha. Ni mara ngapi mnashuhudia wananchi wanafanya shughuli za ujenzi katika maeneo ambayo hawatakiwi halafu mnaenda kuwavunjia badala ya nyie kuwajibika kabla ya kufanya hivyo? Nawaasa fanyeni kazi kwa uadilifu maana udhaifu wa baadhi yenu unasababisha miji kutopangika vizuri," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema wataalamu hao wana wajibu wa kuhakikisha nchi inakuwa na miji iliyopangwa vizuri.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Mipango Miji, Prof. Wilbard Kombe, alisema mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo wa kutatua changamoto zinazokwamisha utekelezaji wa majukumu yao ambazo zimeainishwa kwenye utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha Ardhi. Mkuu wa Shule Kuu ya Mipango Miji katika Chuo Kikuu cha Ardhi, Dk. Ally Namangaya, alisema utafiti huo ulifanyika ili kujua ni kwa nini utekelezaji wa mipango miji ni mdogo katika maeneo mbalimbali nchini.

Alifafanua kuwa kilichoonekana ni kutokuwapo kwa ushirikiano wa wadau wa taasisi za serikali licha ya kuwa sheria kuruhusu.

"Wadau kama wa maji, miundombinu na umeme wamekuwa hawashiriki, wakiitwa hawaji au wanatuma na hali hiyo imesababisha mipango inaenda tofauti kwa taasisi tofauti tofauti za miji. Pia sababu nyingine ni kutokuwapo kwa usimamizi wa ardhi na maendeleo ya mipango miji," alisema.



Meneja Biashara na Masoko wa kampuni ya sukari ya Kilombero, Warda Kimaro (kulia), akiwaonyesha baadhi ya wafanyabiashara, sukari yenye ujazo mpya wa kilo tano, baada ya kuizindua, jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Katibu Mkuu ageukia maendeleo ushirika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, ameitaka Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) kuendelea kuimarisha sekta ya ushirika katika nyanja za kilimo, ufugaji, uvuvi, madini ili ziendelee kuchangia uchumi wa taifa.

Kauli hiyo aliitoa jana katika kikao cha makamishna na watumishi wa tume hiyo jijini hapa, huku akibainisha kuwa umuhimu wa sekta hizo umetokana na kuwaunganisha wanachama katika uzalishaji, ukusanyaji mazao na upatikanaji wa masoko.

Kusaya alisema serikali kupitia tume hiyo imefanya na inaendelea na jitihada mbalimbali za kuimarisha ushirika nchini.

"Serikali imejikita katika kuimarisha usimamizi na utawala bora katika vyama vya ushirika kupitia Sheria ya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013 na kanuni za mwaka 2015 na serikali imeendelea kuchukua hatua kupitia vyombo vya usalama pale ambapo kuna wizi na ubadhirifu kwenye vyama," alisema.

Pia alisema kumekuwapo na mabadiliko chanya kwenye ushirika na kwamba wananchi wameendelea kuanzisha na kujiunga katika vyama ili kupanua shughuli zao.

"Pia kwa sasa wakulima wanauza mazao yao kupitia mfumo wa ushirika, mfumo ambao umesaidia kuimarisha ubora wa mazao, kupatikana kwa bei za ushindani, uhakika wa vipimo vya mazao," alisisitiza Katibu Mkuu.

Alibainisha kuwa mfumo wa ushirika umesaidia upatikanaji wa takwimu sahihi za uzalishaji na uhakika wa mapato ya mamlaka za serikali za mitaa husika.

"Kwa kushirikiana na Soko la Bidhaa (TMX) na bodi za mazao, masoko ya mazao ya kimkakati na mazao mchanganyiko yameendelea kuimarika kama vile mazao ya tumbaku, choroko, kahawa, pamba, ufuta, kokoa na mbaazi yaliuzwa kupitia mfumo wa ushirika katika msimu wa 2019/20 kwa thamani ya Sh. trilioni 2.7," alisema.

Akiwasilisha mafanikio na kero za tume, Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa TCDC, Dk. Benson Ndiege, alisema vyama vya ushirika wa akiba na mikopo (SACCOS) vimeongeza mikopo kwa wanachama wake kutoka Sh. bilioni 854 mwaka 2017 hadi Sh. trilioni 1.5 mwaka jana.

"Tume imeendelea kusimamia masuala ya ajira na kuwezesha wananchi zaidi ya 90,090 kupata ajira katika vyama vya ushirika zikiwamo ajira za kudumu, mkataba na za msimu hadi kufikia Juni 2020 ikilinganishwa na ajira 32,668 mwaka 2018," alisema Dk. Ndiege.

Naye Kamishna Salome Tondi alisema sekta ya ushirika inaweza kuendelea kukua na kuimarika kwa kuhakikisha elimu ya ushirika inawafikia wengi katika jamii.

## Waandishi mitandao wakumbushwa maadili

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

WAANDISHI wa habari mitandao ya kijamii wametakiwa kuzingatia maadili ya uandishi wa habari kwa kuandika habari za ukweli na uhakika ili kuepusha upotoshaji na kujiingiza katika migogoro.

Rai hiyo ilitolewa jana jijini hapa na Wakili wa Kujitegemea James Marenga wakati wa kikao cha tathmini ya Mradi wa Utetezi na Ushawishi wa Haki za Binadamu kwa Kutumia Takwimu (DDA) unaotekelezwa na waandishi wa habari wa vyombo vya habari mbadala kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Alisema waandishi wa habari wa mtandaoni wanapaswa kuzingatia weledi kwa sababu wao wamekuwa wakiripoti matukio papo hapo mara tu matukio yanapotokea.

"Kama unaandika habari mtandaoni suala la maadili ya uandishi wa habari ni muhimu sana na haliepukiki, mnatakiwa kuwa mstari wa mbele kusimamia maadili ya uandishi wa habari ikiwamo kuandika habari za ukweli na uhakika ili kuepuka kujiingiza katika matatizo," alisema Marenga.

Pia aliwahimiza kutochanganya uandishi wa habari na siasa huku akisisitiza kuwa endapo mwandishi wa habari anataka kujihusisha na masuala ya siasa anatakiwa kuacha uandishi wa habari.

Naye Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Arusha (APC) ambaye ni msimamizi wa mradi, Claud Gwandu, aliwataka waandishi hao kufuata sheria zilizopo hata kama hawakubaliani nazo wakati asasi zao zikiwasiliana na serikali kuangalia namna bora ya kurekebisha sheria hizo. Awali, Mwenyekiti wa Waandishi wa Vyombo vya Habari Mbadala (Alternative Media) kupitia mradi huo, Midraji Ibrahim, aliwasisitiza waandishi wa habari kuzingatia maadili ya uandishi wa habari hususani katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu.

Ofisa Mipango wa APC, Seif Mangwangi, alisema kikao hicho ni sehemu ya utekelezaji wa mradi huo kupitia vyombo hiyo na unaofadhiliwa na Mfuko wa Maendeleo wa Watu wa Marekani kupitia Taasisi za Freedom House na PACT na unasimamiwa na APC.





# H'shauri yanunua nyumba 20 za watumishi

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya imenunua nyumba 20 zenye thamani ya Sh. milioni 990 kutoka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Kata ya Lugelele kwa ajili ya watumishi wake.

Akikabidhi nyumba hizo, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali Reuben Mfune, alisema zitasaidia watumishi kuishi kwa utulivu na kutimiza majukumu yao ipasavyo.

Alisema halmashauri ilikubali kuingia makubaliano na NHC kulipa nyumba hizo kuanzia mwaka 2015 hadi 2020 na ndani ya wiki moja kuanzia sasa watumishi wote wanaostahili kuingia wahamie haraka.

Aliongeza kuwa kipaumbele cha kwanza katika ugawaji wa nyumba hizo ni kwa watumishi wa Idara ya Afya wanaotoa huduma katika hospitali mpya ya wilaya kwa ambayo ipo kilometa 1.5 kutoka zilipojengwa nyumba hizo na zitakazobaki wapatiwe watumishi wa idara nyingine za halmashauri.

Mfune aliahidi kuongea na wahusika akiwamo Meneja wa LATRA Mkoa wa Mbeya pamoja na Meneja wa TARURA Wilaya ya Mbarali ili kuratibu na kutengeneza barabara itakayowafikisha wananchi hospitali kwa urahisi kupata huduma za afya.

"Tunajivunia kukamilisha nyumba hizo ambazo ujenzi wake umedumu kwa miaka sita tulingia mkataba na NHC kujenga nyumba 20 zenye thamani ya Sh. milioni 990 ili kupunguza tatizo la uhaba wa makazi kwa watumishi wa halmashauri yetu, baada ya kuhamia walengwa tutaanza kushughulikia suala la miundombinu ya barabara ili wananchi wanaokwenda hospitali mpya ambayo iko jirani na nyumba hizo wasipate shida ya usafiri," alisema Mfune.

Ofisa Mipango wa halmashauri ya wilaya hiyo, Emmanuel Kishimbo, alisema imenunua nyumba hizo kwa Sh. milioni 990 na hadi sasa wamelipa Sh. milioni 100 na wamepanga kulipa Sh. milioni 50 ambazo ni makusanyo ya ndani kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na mwaka wa fedha 2020/2021 halmashauri imetenga Sh. milioni 150 ili kuendelea kulipa deni. Kishimbo aliishukuru NHC kwa kuiwezesha halmashauri kujenga nyumba hizo 20 ambazo zipo jirani na ilipojengwa hospitali mpya ya wilaya ambayo kwa sasa imeanza kutoa huduma za utawala, huduma za uzazi wa mpango, za kinamama na watoto, ustawi wa jamii, lishe pamoja na uhifadhi wa dawa.

Meneja wa NHC Mkoa wa Mbeya, Said Bungala, alisema walijenga nyumba hizo ikiwa kutekeleza wajibu wao wa kuhakikisha wananchi wanapata nyumba za makazi na biashara na katika eneo la Igawa wamefanikiwa kujenga nyumba 20, moja imegharimu Sh. milioni 49.5. Halmashauri imetenga nyumba 12 kwa ajili ya watumishi wa idara ya afya na nyumba nane zinazobaki zitagawanywa kwa watumishi wa idara nyingine.




Meneja wa Taasisi ya Tulia Trust, Jacqueline Boaz (kulia), akigawa vizibao kwa madereva bodaboda wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya juzi, baada ya kukabidhi mkopo wa pikipiki 21 zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 50, lengo ni kuhakikisha madereva hao wanamiliki vyombo vyao vya usafiri ili kujikwamua kiuchumi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Taasisi ya Tulia yatoa mkopo bodaboda 21

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TAASISI ya Tulia Trust imetoa mkopo wa bodaboda 21 zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 50 kwa vikundi mbalimbali vya waendesha bodaboda katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Akikabidhi mkopo huo jana, Meneja wa Tulia Trust Jacqueline Boaz, alisema ni utaratibu kwa taasisi hiyo kuendelea kuwasaidia wananchi wa Jiji la Mbeya kujikwamua kiuchumi hususani vijana.

Boaz alisema baadhi ya vijana wa bodaboda walianza na mkopo wa Sh. 200,000 baada ya marejesho kuwa mazuri walikopa Sh. 800,000 na kuwawezesha kupata fursa ya kukopa vyombo vya usafiri ikiwamo bodaboda na Bajaj.

"Kupitia Taasisi ya Tulia Trust tumewasaidia wananchi wa maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya kujikwamua na umaskini kwa kupata mitaji na kufanya shughuli za kuwaingizia kipato ndio maana siku hizi vitendo vya uhalifu viwamo wizi vimepungua kwa sababu watu wako bize kujitafutia ridhiki naamini tutaendelea kutoa mikopo ya fedha na vyombo vya usafiri ili vijana waweze kutimiza ndoto zao," alisema Boaz.

Akipokea mkopo huo kwa niaba ya wanachama, Mwenyekiti wa Bodaboda jijini hapa, Aliko Fwanda, aliishukuru taasisi hiyo kwa kutoa mikopo yenye riba nafuu ambayo imesaidia kumiliki pikipiki za kwao badala ya kuendelea kuendesha pikipiki za watu.

Mmoja wa wanufaika na mkopo huo, Paul Christopher, alisema wamekubaliana kurejesha mkopo huo kwa wakati ili kutoa fursa kwa wengine kupata fursa hiyo.

Vituo vilivyopatiwa mkopo huo na idadi ya bodaboda kwenye mabano ni Sae (5), Igawilo (6), Stendi Kuu (2), Mwanjelwa (1), Ilomba bodaboda (5) na Iyunga (5).

## RC ataka utaratibu kukopesha vyombo vya moto

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameutaka uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kuanza utaratibu wa kuwakopesha wakulima na vikundi vya wajasiriamali magari ya kusafirisha abiria, matrekta na pawatila ili wawezesha kuongeza uzalishaji na kipato kitakachowawezesha kupata faida na kurudisha mkopo kwa haraka.

Alitoa wito huo hivi karibuni wakati akikabidhi mkopo wa Sh. milioni 243 kwa ajili ya vikundi vya vijana, wenye ulemavu na wanawake.

Alisema ni wakati sasa kwa halmashauri ya wilaya hiyo, kuacha kukopesha vitu vidogo kwa wajasiriamali badala yake wakopeshe fedha au vifaa ambavyo vitasaidia kujiongezea kipato.

"Tupige hatua sasa kutoka hapa tulipo hadi kukopesha vitu vya maana ambavyo vitabadili maisha yetu, vikundi vya bodaboda vikopeshwe angalau Coaster na wakulima wapewe mapawatila na matrekta ili kuongeza ufanisi na uzalishaji wa mazao yao, naipongeza halmashauri ya wilaya kwa kuwa miongoni mwa zinazotoa mikopo mingi kwenye vikundi cha muhimu sasa ni kuongeza thamani ya mikopo hiyo," alisema Chalamila.

Aliwakumbusha vijana kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha walizokopeshwa kwa kuhakikisha wanatumia kwa malengo yaliyokusudiwa badala ya kuhonga na kuongeza nyumba ndogo na hatimaye kushindwa kurudisha mikopo.

Akifafanua mchanganuo wa Sh. milioni 243 kwa ajili ya mikopo, Ofisa Maendeleo ya Jamii, Zena Kapama alisema kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia Machi hadi Juni jumla ya vikundi 26 viliomba mikopo na kati ya hivyo 16 vilikidhi vigezo ambavyo ni wanawake saba, vijana nane na wenye ulemavu kimoja.

Alisema kati ya vikundi hivyo 16 vilivyopata fursa ya mkopo huo vina jumla ya wanakikundi 195 kati yao wanawake 70 na vijana 120 na wenye ulemavu watano na tayari vilipewa elimu ya matumizi sahihi ya mkopo huo ili kupata faida.

"Vikundi hivi 16 ambavyo vimenufaika na mkopo vinajishughulisha na miradi mbalimbali kama vile bodaboda, uzalishaji wa miche ya parachichi, uchanaji na uuzaji wa mbao, uuzaji wa pembejeo za kilimo cha bustani ya kitalu nyumba, ufugaji wa kuku na biashara ya mazao," alisema Kapama.





Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ anayeshughulikia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Khalid Abdalla Omar, akizungumza wakati akifungua mkutano kuhusu Mkakati wa Uwasilishaji wa Afya ya Jamii, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# 'Jifunzeni udahili kujiunga vyuo vikuu'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pemba Juma, amewataka wanafunzi wanaotarajia kujiunga na elimu ya juu kuitumia vizuri fursa waliyoipata ya wiki ya elimu ya juu kujifunza namna ya udahili wa vyuo vikuu unavyofanyika.

Akizungumza jana wakati akifungua Wiki ya Elimu ya Juu, katika viwanja vya Mapinduzi Square Kisonge, alisema iwapo wanafunzi watapata taaluma nzuri ya kujiunga na vyuo vikuu itaondoa tatizo la usajili wa wanafunzi ambao hawana sifa za kujiunga na vyuo hivyo.

Alisema kuwa hali hiyo pia itasaidia wanafunzi kujua vyuo ambavyo vimesajiliwa na vinatambulika kisheria kupitia Bodi za Usajili wa Vyuo Vikuu, TCU na NACTE. Alisema kupitia wiki hiyo, wanafunzi watafahamu namna ya kupata mikopo na masharti yake kwa wale wanaohitaji kuendelea na masomo ambao hawana uwezo wa kujisomesha. Aliwataka kuwa mabalozi wazuri kwa wenzao kutokana na taaluma waliyoipata kuwahamasisha na wengine ili lengo la kutoa elimu hiyo liweze kufikiwa.

Aliwapongeza wafadhili mbalimbali waliojitokeza kuchangia kufanikisha shughuli hiyo na kuwaomba kuendelea kutoa kwa lengo la kusaidia harakati za kielimu nchini.

Naye Naibu Katibu Mkuu Taaluma Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Madina Mjaka Mwinyi, aliwataka wanafunzi kuitumia vyema fursa hiyo ili waweze kupata elimu ya juu ya Taasisi za Elimu ya Juu na kujua fani zinazotolewa katika vyuo mbalimbali.

Mkuu wa Kitengo cha Elimu ya Juu Sayansi na Teknolojia, Aida Juma Maoulid, alisema kuwa kupitia tamasha hilo wanafunzi watafahamu namna ya kufanya udahili wa kujiunga katika vyuo pamoja na njia sahihi za kupata mikopo ili waweze kujiunga na elimu ya juu.

# Wataalamu afya watakiwa kushirikiana watoa huduma

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Khalid Abdalla Omar, amewataka wataalamu wa afya kushirikiana na kuwasimamia wahudumu wa afya wa kujitolea ili kutekeleza vyema majukumu yao.

Aliyasema hayo jana katika hafla ya ufunguzi wa uwasilishwaji wa mkakati wa afya ya jamii uliofanyika mjini hapa.

Alisema wahudumu wa afya wa kujitolea wana mipaka yao katika utekelezaji wa kazi zao hivyo ni vyema wakahakikisha kwamba wanasimamiwa ipasavyo katika kufanikisha majukumu yao.

Alisema sio vizuri kuachiwa kufanya majukumu yasiyowahusu ili kujiepusha kupata madhara kwa jamii. "Wahudumu wa afya wa kujitolea wana mipaka yao katika utekelezaji wa kazi zao naomba sana tuwasimamie kutekeleza majukumu yao bila ya kukiuka mipaka ya kuwatumia kufanya majukumu ya wataalamu wa afya," alisema.

Pia, alisema iwapo watawatumia ipasavyo wahudumu hao watasaidia kuimarika huduma za afya kwa jamii pamoja na kufikisha kwa ukaribu.

"Tukiwatumia ipasavyo tutakuwa tumeifikia jamii kwa karibu sana na hilo litafanya afya za Wazanzibari kuimarika," alisema.

Mkurugenzi wa Kinga kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja, Fadhil Mohamed Abdalla, aliwasisitiza wahudumu hao kufuata sheria na kanuni za mkakati huo kwa lengo la kuimarisha utoaji wa huduma ya jamii na kupata taifa lenye vijana imara. Washiriki hao wamepongeza kuanzishwa mkakati huo na kuahidi kutekeleza vyema majukumu yaliyowekwa ili kutoa huduma bora na kuzidi ubora wa uimarishaji wa huduma hiyo kwa jamii.

# ADA TADEA yajipanga kampeni za kistaarabu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MGOMBEA urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha ADA TADEA, Juma Ali Khatib, amesema chama chake kimejipanga kufanya kampeni za kistaarabu zitakazozingatia maadili na kanuni za uchaguzi kwa ajili ya kujenga mshikamano na kudumisha amani na utulivu.

Khatib alisema hayo kufuatia wajumbe wa mkutano mkuu wa chama hicho uliofanyika jijini Dar es Salaam juzi kumchagua kwa kupata kura 126 kati ya kura zote zilizopigwa 130 na kuwa mgombea wa nafasi ya urais wa Zanzibar katika uchaguzi mkuu.

Akizungumza na Nipashe baada ya kuwasili Zanzibar katika ofisi ya chama hicho Mombasa kwa Mchina, Khatib alisema chama chake kimejipanga kufanya kampeni katika uchaguzi mkuu za kistaarabu kwa mujibu wa makubaliano ya kanuni za uchaguzi mkuu.

Alisema chama chake kimezingatia harakati za kampeni kumalizika kwamba maisha yapo kama kawaida kwa hivyo hakuna sababu ya kusababisha malumbano, mifarakano na uhasama unaoweza kuhatarisha amani na mshikamano wa taifa.

"Chama chetu kimetia saini makubaliano ya kutekeleza na kusimamia kanuni za uchaguzi yaliyoratibiwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC), kwa hivyo tunaahidi kufanya kampeni zitakazojenga umoja na mshikamano bila ya kutukanana katika majukwaa ya kisiasa," alisema.

Alisema mambo ya msingi ambayo yanakusudiwa kutekelezwa na chama hicho katika kipindi cha kampeni za uchaguzi mkuu ni kuendeleza kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati iliyosimamiwa na Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein.

Alitaja miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa bandari kubwa ya kisasa ya Mpiga duri iliyopo Maruhumbi mjini Unguja pamoja na bandari ya kuhifadhi mafuta ambayo ujenzi wake unaendelea huko Mangapwani, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema wajawazito watakapojifungua watapewa fedha za kujikimu kwa ajili ya matunzo ya watoto wao kwa kupata makuzi bora na afya njema.

"Hiyo ndiyo mikakati yetu ya utekelezaji wa ilani...tutatekeleza na kumaliza miradi ambayo imeachwa na Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein, ikiwamo ujenzi wa bandari ya Mpigaduri na bandari ya kuhifadhi mafuta iliyopo Mangapwani Mkoa wa Kaskazini Unguja," alisema.

Naibu Katibu Mwenenzi wa ADA TADEA, Rashid Mshenga, alisema wamefurahishwa na ushindi mkubwa alioupata mgombea wao ikiwa ni ishara kwamba anakubalika katika chama na wanachama.

"Chama cha ADA TADEA sasa kipo tayari kwa ajili ya kushiriki uchaguzi mkuu wa Oktoba kwa nafasi ya urais baada ya kupata mgombea atakayepeperusha bendera ya chama chetu," alisema.

John Shibuda pia amechaguliwa kuwa mgombea wa nafasi ya urais wa Jamhuri ya Muungano baada ya kupata kura 120.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL,** Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile: **Kuboresha biashara, Kulipa kodi ya nyumba, Kumalizia tenda, Kulipa ada, Kulipa matibabu n.k.**
**Mawasiliano** yetu **Dar es salaam** – 0768 928 516. **Arusha** – 0677 226 960.


## NIPASHE NI JIBU LAKO

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676**


---

**Notice/summons to appear (O.V.R.20 (1) of (CPC)**
**(Substituted Service)**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**LAND APPEAL NO. 26 OF 2019**
**MOSES MOMBA......................... APPELANT**
**VERSUS**
**HASFA HAMIS..................................1ST RESPONDENT**
**HANANGU MASHAURI.............................2ND RESPONDENT**

TO: HANANGU MASHAURI…..2ND RESPONDENT

WHEREAS; The above named Appellant has instituted an appeal against you; you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or agent duly authorized on 16th day of September, 2020 at 09:00 am before Hon. M. Opiyo, J (Chamber No. 5) to answer the said appeal; and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your defence.

TAKE NOTICE that, in default of your appearance on that day before mentioned, the appeal will be heard and determined in your absence.

Given under my Hand and the seal of this court, this 01 day of July,2020.

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
LAND DIVISION

158326

---

**DAR ES SALAAAM**
**SHAURI LA MADAI NO 144 YA MWAKA 2020**

**SAID ….ALLY…. ABDALLAH…. MDAI**
**NAYAZ… NA ZIM… BANJI …MDAIWA**
**KWA**
**MHARIRI GAZETI**
**LA NIPASHE**
**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ambayo maelezo ya mdai yameelezwa katika nakala ya madai ambazo zinaweza kujulikana katika mahakama hii, kwa hiyo mnahitajiwa kuhudhuria katika mahakama hii binafsi au kwa wakili au mwakilishi ambaye anaruhusiwa, siku ya tarehe 30/7 saa 2:30 asubuhi. Kwa mujibu wa madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukata shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

**ANGALIA**

Kama hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama ikithibitisha kama mmepokea kuitwa shauri ni, itaweza kutoa hukumu kuwa mmeshindwa
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 20 mwezi 07/2020

---

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MINISTRY OF HOME AFFAIRS
IMMIGRATION DEPARTMENT



Hii ni taarifa kwamba:
REHEMA ALI WAKATI
P.O BOX 78300
DAR ES SALAAM.
OMBI LA URAIA WA TANZANIA

Mwenye picha hapo juu, anaomba uraia wa Tanzania kwa Mh. Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Utaifa wake wa sasa ni KENYA. Nchi atokayo ni KENYA. Yupo hapa nchini tangu 2007.

Kwa yeyote mwenye taarifa/sababu za kwanini mwombaji asipewe Uraia wa Tanzania, atume taarifa ya maandishi kwa Kamishna Jenerali wa Uhamiaji S.L.P 512, Dar es salaam. Kumb Na. DN.75792

HASSAN A.M
FOR: COMMISSIONER GENERAL OF IMMIGRATION

---

## KUPOTEA KWA VYETI



Ally Suedy anatangazakupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0110-0003 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Tanzania mwaka 2001 katika shule ya Sekondari Ilboru.

Yeyote atakakiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa:
KMR/RB/7491/2012

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**Magesa Samwel** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo , kidato cha nne chenye index namba S.1020-0025 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Tanzania mwaka 2003 katika shule ya Sekondari Machochwe, Cheti cha kidato cha sita chenye index namba P0333/0656 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2008 katika shule ya Sekondari Mwanza, Cheti cha Ualimu chenye index namba E0523-0047 kilichotolewa na Chuo cha Ualimu Monduli mwaka 2005.

Yeyote atakakiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa: DSM/PHQ/RB/559729/2020.

---

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MWANZA**

**SHAURI LA ARDHI RUFAA NAMBA 54 YA MWAKA 2016**

**NEEMA MUNUO URASA......................MRUFANI**

**DHIDI YA**

**MUSA BISIMWA PAUL.....................MRUFANIWA**

**KWA: MUSA BISIMWA PAUL**

**KUITWA SHAURINI**

Unaarifiwa kuhudhuria hapa mahakamani tarehe 03/08/2020 kuja kusikiliza shauri la ardhi rufaa iliyofunguliwa na mrufani dhidi yako
Unatahadharishwa kuwa endapo hautofika siku hiyo shauri hili litasikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa maamuzi.
Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya mahakama leo tarehe 22/7/2020.

NAIBU MSAJIRI
MAHAKAMA KUU TANZANIA
MWANZA

---

**Notice/summons to appear (O.V.R.20 (1) of (CPC)**
**(Substituted Service)**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**

**LAND APPEAL NO. 26 OF 2019**

**MOSES MOMBA......................... APPELANT**

**VERSUS**

**HASFA HAMIS..................................1ST RESPONDENT**
**HANANGU MASHAURI.............................2ND RESPONDENT**

**TO: HANANGU MASHAURI.....2ND RESPONDENT**

**WHEREAS;** The above named Appellant has instituted an appeal against you; you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or agent duly authorized on 16th day of September, 2020 at 09:00 am before Hon. M. Opiyo, J (Chamber No. 5) to answer the said appeal; and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your defence.
**TAKE NOTICE** that, in default of your appearance on that day before mentioned, the appeal will be heard and determined in your absence.
Given under my Hand and the seal of this court, this 01 day of July,2020.

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
LAND DIVISION

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MOROGORO .**

**MAOMBI NA: 59 YA MWAKA 2020.**

**EDOM ELIAS MWAKITENGA........MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**AMINA SHOMARI MHOMBA.........MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA AMINA SHOMARI MHOMBA.**

Popote ulipo unaarifiwa ufike ktk baraza la ardhi na Nyumba la wilaya ya Morogoro tarehe 27/08/2020.Wewe mwenyewe binafsi au mtume mwakilishi wako bila kukosa ambapo MAOMBI yamepangwa kutajwa. Endapo hautaudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imetolewa kwa mkono wangu Leo tarehe 28 mwezi 07 mwaka 2020.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI.

**Abel C. Rwebangira** amepotelewa na kadi ya gari namba **T 434 CWM** aina ya Canter. Taarifa za kupotea kwa kadi zipo kituo cha Polisi Bukoba **KG/BK/RB/205778/2020.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**ULIMWENGU KAGOMA JUMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.4218/0229 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia REV. A. BUNGWA SEKONDARI mwaka 2014.

**Cheti cha JKT na Cheti cha Darasa la Saba kilichotolewa na Shule ya Msingi MUDYANDA mwaka 2010.**

**Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.**
**Taarifa ya polisi: MKU/RB/433/2020.**

---

IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
AT BUKOBA
LAND APPEAL NO. 72/2019
MUNICIPAL DIRECTOR BUKOBA MUNICIPAL COUNCIL
............APPLICANT
VERSUS
HANIFA JUMA ......................RESPONDENT

TO, HANIFA JUMA
C/O WEO - KASHAI WARD BUKOBA

**RE: NOTICE OF DATE FOR HEARING**

Whereas the above Applicant lodged a case registered as Land appeal no 72/2019 against you at the High Court of Tanzania at Bukoba.

Take notice that the above said Case has been scheduled for hearing on 21st day of September, 2020 at 9:00 am before Hon. Judge N.N. Kilekamajenga. You are authorized to appear in person or through your Advocate.

Take further notice that in default of your appearance on that date and time for the saidi hearing the case may proceed in your absence.

Given under my hand and seal of this Court this 20th day of July 2020.

J. M. MINDE
DEPUTY REGISTRAR
BUKOBA

158337

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya CHAMWINO MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 66/2020**

Ombi la ZUWENA MOHAMED OMARI kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu MOHAMED OMARI

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 17/08/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 23/07/2020.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
CHAMWINO MJINI
DODOMA.

158327

---


***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0782253676***

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

MuCoBa

# MUCOBA BANK PLC

P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075
Mafinga, Tanzania.

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30/6/2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya/Mwaka wa sasa 6/30/20 | Robo Mwaka/Mwaka iliopita 3/31/20 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslim | 701 | 674 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu Ya Tanzania | 327 | 269 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio katika Benki Nyingine na Taasisis za Fedha | 1,498 | 1,856 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizo afikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizo kubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki nyingine | - | - |
| 10 | uwekezaji katika Amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 11,809 | 10,730 |
| 12 | Mali nyingine | 3,005 | 4,269 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa. | 369 | 391 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **17,709** | **18,189** |
| | | | |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisis za Fedha | 3 | 3 |
| 18 | Amana za Wateja | 15,191 | 15,590 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 95 | 95 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Benki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 257 | 39 |
| 24 | Dhima la Tozo KWA Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi. | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 203 | 670 |
| 28 | Madeni | 2,946 | 2,946 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **18,695** | **19,343** |
| 30 | **MALI(DHIMA) HALISI (16 Kutoa 29)** | **(986)** | **(1,154)** |
| | | | |
| | | | |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 2,764 | 2,764 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (4,203) | (4,203) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 343 | 175 |
| 35 | Akaunti nyingine za Mtaji | 111 | 111 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEHDA ZA WANAHISA** | **(986)** | **(1,154)** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 0 | 0 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 1011 | 960 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 563 | 774 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 0 | 0 |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Amana | -5.57% | -6.34% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo ghafi | 8.17% | 8.35% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 77.74% | 68.82% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 66.68% | 58.99% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zilizozalisha na Jumla ya Mali | 85.37% | 73.50% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -2.56% | 6.87% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -2.64% | 6.56% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30/06/2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa 6/30/20 | Robo ya mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 6/30/19 | Limbikizo lamwaka sasa 6/30/20 | Limbikizo la mwaka linganishi (mwaka uliopita) 6/30/19 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 1,020 | 704 | 1,851 | 1,507 |
| 2 | Gharama za Riba | 245 | 157 | 384 | 365 |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | 775 | 547 | 1,467 | 1,141 |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 92 | 43 | 100 | 78 |
| | | | | | |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **191** | **320** | **374** | **484** |
| | 6.1 Faida/ (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 155 | 152 | 273 | 256 |
| | 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 6.4 Mapato Mengine | 36 | 168 | 101 | 228 |
| 7 | **Gharma Zisizo za Riba:** | **706** | **663** | **1,398** | **1,383** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 341 | 270 | 648 | 546 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 21 | 59 | 32 | 113 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 344 | 334 | 718 | 725 |
| 8 | **Faida/ (Hasara) ya Uendeshaji** | **168** | **162** | **343** | **164** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 50 | 49 | 103 | 49 |
| 10 | **Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **118** | **162** | **240** | **115** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **118** | **162** | **240** | **115** |
| 13 | Idadi ya waajiriwa | 56 | 53 | 58 | 53 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 42.09 | 20.24 | 21.46 | 23.08 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | | | | | |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na wastani wa mali | 0.94% | 0.86% | 1.91% | 0.87% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya kodi na wastani wafedha za wanahisa | -15.70% | 5.83% | -32.07% | 5.91% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya riba na mapato ghafi | 58.31% | 64.72% | 62.83% | 69.48% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya riba na wastani wa mali zinazozalisha | 3.95% | 2.56% | 7.48% | 5.34% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30/06/2020

| | Mtaji wa hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la zaidi ya jumla | Mengineyo Bainisha | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **2,764** | - | **(4,203)** | **24** | **87** | - | **(1,328)** |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 343 | - | - | - | **343** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na Wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **2,764** | - | **(3,861)** | **24** | **87** | - | **(986)** |
| | | | | | | | |
| **Mwaka Uliopita 2019** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | **2,748** | - | **(5,556)** | **504** | **88** | **1** | **(2,215)** |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 409 | - | - | - | **409** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | 944 | (480) | (1) | (1) | **462** |
| Mengineyo | 16 | - | - | - | - | - | **16** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **2,764** | - | **(4,203)** | **24** | **87** | **(0)** | **(1,328)** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 31-03-2020
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa 6/30/20 | Robo ya Mwaka iliyopita 3/31/20 | Limbikizo la mwaka wa sasa 6/30/20 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 6/30/19 |
|---|---|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za uendeshaji** | | | | |
| | Mapato/ (Hasara) Halisi | 168 | 175 | 343 | 164 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| | Hasara Katika Mali | 136 | 54 | 190 | 127 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,079) | (270) | (1,349) | 115 |
| | Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | (399) | 1,097 | 698 | 1,302 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko halisi Katika Dhima Nyingine | (249) | (52) | (301) | 215 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 1,264 | (352) | 912 | (687) |
| | Kodi Iliyolipwa | (105) | (20) | (125) | (63) |
| | Mengineyo (Bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli** | **(264)** | **632** | **368** | **1,172** |
| | **Zauendeshaji** | | | | |
| | | | | | |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana** | | | | |
| | **na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (9) | - | (9) | (37) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya mali zakudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya amana Zisisoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa** | **(9)** | **-** | **(9)** | **(37)** |
| | **(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | | | | |
| | | | | | |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za kifedha** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | (99) | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutoka na Utoaji wa mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | (1) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | (360) |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | (89) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika)** | **-** | **-** | **(99)** | **(450)** |
| | **Kwa shughuli zakifedha Kifedha** | | | | |
| | | | | | |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu.** | | | | |
| | Ongezeko /Punguzo Halisi Katika | - | - | - | - |
| | Fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu | (273) | 533 | 260 | 686 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mw | 2,799 | 2,266 | 2,266 | 2,430 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa Robo Mwaka/Mw | **2,526** | **2,799** | **2,526** | **3,116** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA

**Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, Sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita ( kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)**

| *Jina Na Cheo* | *Saini* | ***Tarehe*** |
|---|---|---|
| Philipo Raymond ……………………………… Meneja Mkuu | (Imesainiwa) | **30/Jul/2018** |
| Kelvin Mushi …………………………………… Meneja wa kitengo cha Fedha and Utawala | (Imesainiwa) | **30/Jul/2020** |
| Hilda Valerian…………………………………… Mkaguzi Mkuu wa Ndani | (Imesainiwa) | **30/Jul/2020** |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunadhibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa za uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonyesha hali halisi**

| **Jina** | **Tarehe** |
|---|---|
| 1. Prof.Domicus Kasilo………………………… (Imesainiwa) Mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi | 30/Jul/2020 |
| 2. Bw.Kitova Mungai ……………………………… (Imesainiwa) Mkurugenzi | 30/Jul/2020 |

### MUCOBA BANK PLC- CHARGES AND FEES- 2020

| SAVINGS ACCOUNT | CHARGES AND FEES |
|---|---|
| **Individual Savings Account** | |
| Account opening minimum amount | 20,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Credit Interest Rate | 2% |
| | |
| **Joint Savings Account** | |
| Account opening minimum amount | 20,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Credit Interest Rate | 2% |
| | |
| **Juvenile's/ Minor Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Biashara Savings Account** | |
| Account Opening minimum amount | 65,000 |
| Minimum operating balance | 50,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 50,000 |
| Monthly Service Fee | 5,000 |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Group Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Saccos Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 55,000 |
| Minimum operating balance | 50,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 100,000 |
| Monthly Service Fee | 2,000 |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Elimu Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 10,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Malengo Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 5,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | See Table below |

**Malengo account interest rates are as follows:**

| Period | | Rate |
|---|---|---|
| 3 months | | 4% |
| 6 months | | 5% |
| 12months | | 6% |

**FIXED DEPOSIT ACCOUNTS**

| Period | Range | Rate |
|---|---|---|
| 3 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 4.00% |
| 6 months | Up toTzs 9,999,999.00 | 4.50% |
| 9 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 5.00% |
| 12 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 6.00% |
| 24 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 7.00% |
| 36 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 8.00% |

FDR of Tzs **10,000,000** and above is **negotiable** at management discretion.

**GENERAL CHARGES AND FEES**

| GENERAL CHARGES/ FEES | TZS |
|---|---|
| | |
| **Dishonored/Unpaid cheque** | |
| Fund related | NA |
| Technical | NA |
| | |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS** | |
| Cash deposit at branch | Free |
| Cheque clearing (up to Tzs 1,500,000) | 15,000 |
| Cheque clearing (above Tzs 1,500,000) | 1% |
| Cash withdrawal- (less Tzs 5,000,000) | 1,000 |
| Cash withdrawal- (Tzs 5,000,000 and above) | Tzs 1,000 plus 0.08% of excess above 5,000,000, Max |
| | Tzs 150,000 |
| Account closure | 15,000 |
| Dormant account reactivation | 3,000 |
| Dormant account monthly Fee | 1,000 |
| Premature/cancelled Fixed Deposit Fee | No interest given |
| Interim Statement Fee | 1,000 |
| Audit confirmation Fee | 10,000 |
| Balance certificate Fee | 20,000 |
| Reference Letter | NA |
| TT Outward local-TISS | NA |
| TT Outward local- EFT | NA |
| TT Inward local- TISS | NA |
| TT Outward local- EFT | NA |
| Salary Processing (per entry) | 2,500 |
| Bank Guarantees | NA |
| Balancy Inquiry | 100 |
| Money Transfer | 12,000 |
| ATM card replacement | 15,000 |
| ATM w/drawal Fee (on us) | 1,300 |
| To other bank ATMs w/drawal Fee | 1,300 |
| ATM mini statement | |
| Wallet to Bank | 1,000 |
| SMS alart | 1,000 |
| Bank to Wallet (Below Tzs 100,000) | 1,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 100,000-199,999) | 1,300 |
| Bank to Wallet (Tzs 200,000-299,999) | 1,700 |
| Bank to Wallet (Tzs 300,000-399,999) | 2,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 400,000-499,999) | 2,500 |
| Bank to Wallet (Tzs 500,000-599,999) | 3,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 600,000-699,999) | 3,500 |
| Savings account interest rates | 2% |

## TANGAZO

IITA Transforming African Agriculture

CGIAR

# Pumzika kwa Amani

**Mhe Benjamin William Mkapa**
(1938 – 2020)





*Rais mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Mhe. Benjamin Willian Mkapa, katika ufunguzi rasmi wa ofisi za IITA-Mashariki mwa Afrika jijini Dar es salaam, Tanzania, mnamo 2013.*

Bodi, menejimenti na wafanyikazi wa Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Kilimo cha Kitropiki (IITA), tunatoa rambirambi zetu kwa Mh. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, familia, marafiki na wa-Tanzania wote, kwa kuondokewa na Rais mstaafu Mh. Benjamin William Mkapa.

IITA tutakumbuka na kuthamini kazi yake ya kuleta mabadiliko katika sekta ya kilimo nchini Tanzania, kwa kuhimiza kilimo kibiashara, ili kuleta maendeleo ya nchi kupitia ajenda yake ya kupunguza umasikini, na kwa kupigania amani Africa ya Mashariki na Kati.

**Mwenyezi Mungu aipumzishe roho yake kwa amani na awape nguvu na uvumilivu wakati huu wa majonzi.**

www.iita.org

## HABARI MICHEZO

# DEMBELE, GRIEZMANN WAANZA MAZOEZI




**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imerudi kwenye mazoezi Jumanne kwa ajili ya kujiandaa na Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku Ousmane Dembele na Antoine Griezmann wakirejea uwanjani.

Wafaransa hao wawili walikuwa nje ya dimba kutokana na majeruhi, lakini sasa afya zao zinaonekana kuimarika.

Griezmann aliumia wakati Barcelona wakishinda 1-0 dhidi ya Real Valladolid Julai 11 na kumlazimisha kukosa mechi mbili za mwisho za LaLiga wakati Barca wakipoteza Kombe kwa Real Madrid.

Dembele yeye alifanyiwa upasuaji baada ya kuumia Februari, mwaka huu na alionekana kama angekaa nje kwa muda mrefu.

Hata hivyo, kusimama kwa msimu wa 2019-20 kutokana na mlipuko wa virusi vya corona kumefanya sasa winga huyo kuwa na uwezekano wa kucheza kweye michuano hiyo ya Ulaya.

Dembele na Griezmann sasa wamerudi kwenye mazoezi ya kikosi cha Barcelona, huku mlinzi Clement Lenglet pia naye akionekana kuwa fiti akitoka kwenye majeruhi.

Barca inajiandaa kuivaa Napoli kwenye mchezo wa pili wa hatua ya mtoano wa timu 16, utakaopigwa Agosti 8, mwaka huu kwenye Uwanja wa Camp Nou.

Kwenye mchezo wa kwanza timu hizo zilitoka sare ya kufungana bao 1-1.




# Lovren asajiliwa rasmi Zenit

**LIVERPOOL** England

MLINZI wa Liverpool, Dejan Lovren amejiunga na miamba wa Ligi Kuu Urusi, Zenit kwa mkataba wa miaka mitatu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 alijiunga na mabingwa wa Ligi Kuu England mwaka 2014 akitokea Southampton na amecheza jumla ya mechi 185 kwa wekundu hao wa Anfield, akifunga mabao nane.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Croatia amefurahia mafanikio katika miaka yake miwili ya mwisho, akishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, UEFA Super Cup, Klabu Bingwa ya Dunia na Ligi Kuu England.

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp aliiambia tovuti ya klabu hiyo: "Gwiji mwingine wa Liverpool ameondoka klabuni, kwa sababu alikuwa mchezaji muhimu sana kwa timu hii.

"Tangu siku ya kwanza, nakumbuka tulipocheza na Borussia Dortmund dhidi ya Liverpool kwenye maandalizi ya msimu kwenye mechi ya kirafiki na Dejan alifunga kwa kichwa.

"Na hiyo ilikuwa taswira yangu kuhusu walinzi wa klabu hii wakati nakuja hapa."

Zenit imeripotiwa kulipa kiasi cha euro milioni 12 ili kumnasa mlinzi huyo wa kati.

# Klabu tano zajitosa kumwania Willian

**LONDON,** England

WILLIAN amepata ofa kutoka timu tano zikiwamo mbili za klabu zinazoshiriki Ligi Kuu England, kwa mujibu wa wakala wa winga huyo wa Chelsea.

Mkataba wa Willian na Chelsea unamalizika mwishoni mwa msimu huu na nyota huyo wa kimataifa wa Brazil ameshindwa kufikia makubaliano ya kuongeza mkataba mpya.

Arsenal ni miongoni mwa timu inayotajwa kumwania winga huyo mwenye umri wa miaka 31, ambaye amebainisha kutaka kubakia jijini London.

Kumekuwa na uvumi kwamba Willian kwa sasa yupo tayari kusaini mkataba wa miaka miwili badala ya mitatu aliyokuwa akiitaka pale Stamford Bridge.

Hata hivyo, wakala wake, Kia Joorabchian amesema hakujawa na mabadiliko kuhusu fikra yake ya kutaka kubakia England kwa sababu tayari kuna klabu mbili zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili na mbili nyingine kutoka Ulaya na moja kutoka Ligi Kuu ya Marekani, MLS.

"Sidhani kama amebadili uamuzi," amesema Joorabchian akiiambia talkSPORT.

"Mara zote amekuwa na hamu ya kuendelea kubakia hapa na kucheza zaidi na zaidi.

"Tumepata ofa kubwa kutoka Ligi Kuu ya Marekani, lakini kwa sasa bado hatujatoa uamuzi wa wapi pa kwenda."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BECKHAM AJITOSA KUMSAJILI SUAREZ

●●● Lengo la kumsajili straika huyo ni kuijenga upya Inter Miami ambayo imeanza msimu...

**MIAMI,** Marekani

KLABU ya Inter Miami ambayo mmoja wa wamiliki wake ni David Beckham, imeonyesha nia ya kumsajili straika wa Barcelona, Luis Suarez akiwa mchezaji huru katika majira ya joto mwakani.

Kama mambo yataendelea yalivyo sasa, Suarez atamaliza mkataba wake na Barcelona ifikapo Julai mwakani na Inter Miami imejiandaa kumpa mkataba wa miaka minne nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Uruguay.

Kwa mujibu wa gazeti la Mundo Deportivo limeandika kuwa ingawa Inter Miami imedhamiria kumsajili Suarez, nyota huyo anaamini Barcelona itafanya uamuzi wa kumwongezea mkataba mpya.

**Kama Suarez anafanikiwa kucheza asilimia 60 ya mechi za Barcelona za msimu ujao, ni wazi mkataba wake moja kwa moja utaendelea.**

Msimu huu, Suarez amefunga mabao 19 na kutoa pasi za mwisho 12 katika mechi 34 alizoichezea Barcelona katika mashindano yote.

Inter Miami inahitaji kusajili wachezaji wapya ili kuimarisha kikosi chake katika msimu mpya wa MLS, huku ikiwa imemaliza mkiani kwenye Ligi ya Kanda ya Mashariki baada ya kupoteza mechi zake tano hadi sasa.

Ingawa Suarez atafikisha umri wa miaka 34 wakati mkataba wake wa sasa na Barcelona utakapomalizika, anaonekana anaweza kwenda kuisaidia kufanya vema katika ligi hiyo ya MLS.

Kwa sasa Suarez anajipanga kuitumikia vema Barcelona, ambayo inajiandaa na mechi ya marudiano ya hatua ya 16 Bora ya Mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Napoli, huku kikosi chake kikilazimishwa sare ya bao 1-1 katika mchezo wa kwanza uliochezwa nchini Italia.

## ZISIKUPITE

### TORRES ANUKIA CITY

MANCHESTER City imeweka wazi inahitaji saini ya winga wa Valencia Mhispani, Ferran Torres (20), katika dirisha la usajili litakalofungiliwa kuelekea msimu mpya. ***(ESPN)***

### HOJBJERG KUTUA SPURS

TOTTENHAM inakaribia kukamilisha mchakato wa kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg (24), kutoka Southampton. ***(Sky Sports)***

### COUTINHO AGOMBEWA ENGLAND

ARSENAL, Tottenham na Leicester zote zimetangaza kupambana kuwania saini ya kiungo wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Brazil, Philippe Coutinho (28), ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Bayern Munich. ***(Sport - in Spanish)***

### CHILWELL AITAJA CHELSEA

BEKI wa kushoto wa Timu ya Taifa ya England, Ben Chilwell (23), wiki hii anajipanga kuieleza Leicester kwamba anataka kuondoka klabuni hapo na kujiunga na Chelsea. ***(Mirror)***

### ATLETICO: OBLAK HAONDOKI

RAIS wa Atletico Madrid, Enrique Cerezo ameondoa uvumi uliokuwa unamhusisha golikipa wa Timu ya Taifa ya Slovenia, Jan Oblak (27), kuwa anajiandaa kuondoka katika klabu hiyo. ***(Marca - in Spanish)***

### EZE ATAKIWA WEST

WEST Ham inajiimarisha katika mchakato wa kuwania saini ya mshambuliaji wa QPR, Eberechi Eze, ambaye ni mchezaji wa Timu ya Taifa ya Vijana ya England (U-21) na thamani yake ikitajwa ni pauni milioni 20. ***(Guardian)***

### LEEDS YAINGIA SOKONI

MABOSI wa Leeds United wamewasilisha ofa ya pauni milioni 15 ili kuwania saini ya beki wa Tottenham na Timu ya Taifa ya Argentina, Juan Foyth, ambaye ana umri wa miaka 22. ***(Sun)***

### CEBALLOS MAMBO SAFI

ARSENAL inakaribia kukamilisha mazungumzo na Real Madrid kwa ajili ya kumpa mkataba mpya Dani Ceballos baada ya kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Hispania mwenye umri wa miaka 23 kuonyesha kiwango kizuri msimu huu akiwa hapo Emirates. ***(Mail)***

### ROMA, UNITED WATETA

ROMA iko tayari kukamilisha mazungumzo na Manchester United ili kumpa mkataba wa kudumu beki wake, Chris Smalling, ambaye ana umri wa miaka 30. ***(Corriere dello Sport - in Italian)***

### SILVA ANUKIA LAZIO

LAZIO iko kwenye mazungumzo na Manchester City ili kumsajili kiungo mchezeshaji Mhispania David Silva, ambaye ana umri wa miaka 34. ***(AS)***

### MADDISON KUJIFUNGA

KIUNGO wa Leicester ambaye ni raia wa England, James Maddison (23), anajiandaa kusaini mkataba mpya wa miaka mitano ambao atakuwa anapokea mshahara wa pauni 100,000 kwa wiki abakie klabuni hapo. ***(Mail)***

HABARI MICHEZO

## Ukata waitesa Marsh Queens

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Marsh Queens, Aaron George amesema sababu kubwa ya timu yake kufanya vibaya kwenye mechi za Ligi Kuu ya Wanawake msimu huu ni kutokana na ukosefu wa fedha waliokuwa nao.

Akizungumza na gazeti hili jana, George alisema suala la kukosa fedha limesababisha baadhi ya viongozi wa timu kujitoa na kufanya maandalizi kutofanyika vema.

Kocha huyo alisema timu hiyo imekuwa katika wakati mgumu hali iliyopelekea kubakia na wachezaji wachache baada ya likizo ya corona kumalizika.

"Kwa sasa tunaenda kwa kumwomba Mungu, timu ina matatizo ya kifedha na wachezaji hasa wakigeni kutoka Kenya tuliokuwa nao mwanzoni mwa msimu, walishindwa kurudi kuendelea na majukumu yao, pia kuna viongozi wamejitoa," alisema George.

Aliongeza kwa upande wa benchi la ufundi bado wanapambana kuhakikisha wachezaji wengine wanne ambao walikuwa nje ya kikosi wanarejea ili timu ifanye vizuri katika mechi zilizobaki za msimu huu.

"Licha ya kuwa katika hali ngumu, nina imani timu yetu itafanya vizuri katika mechi nne za mwisho, ambapo michezo miwili tutacheza nyumbani na miwili tutatoka nje," George alisema.

Alitaja mechi mbili za ugenini zilizobakia ni dhidi ya Panama Queens ya Iringa na baadaye wataifuata Ruvuma Queens mjini Songea halafu watarejea jijini Mwanza kuwasubiri mabingwa watetezi, JKT Queens pamoja na Yanga Princess.

Marsh Queens iko katika nafasi ya pili kutoka mkiani kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 12 baada ya kucheza michezo 18.

## Minziro, Mbao mambo magumu

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Mbao FC inayopambana kujinusuru kubakia Ligi Kuu Tanzania Bara umesema hatima ya Kocha Mkuu wa timu hiyo, Fred Felix Minziro itajulikana baada ya kumalizika kwa mechi ya hatua ya mtoano itakayochezwa Jumamosi.

Minziro aliiongoza vema Mbao FC iliyokuwa mkiani hadi kupata tiketi ya kucheza mechi za mtoano na endapo atashinda, timu hiyo itabakia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Mbao FC, Richard Melli, alisema walimpa Minziro timu hiyo kwa lengo la kuinusuru isishuke daraja, sasa bado wanasubiri kuona mwisho wa kazi waliyompatia.

Melli alisema wana imani na kocha huyo atafanikiwa kuwabakisha kutokana na kiwango walichokionyesha kwenye baadhi ya mechi za Ligi Kuu Bara zilizomalizika hivi karibuni.

Aliongeza Mbao FC inaheshimu kazi na mchango aliofanya kocha huyo na kwa sasa wanaamini anaweza kuwasaidia wasishuke daraja ingawa wanafahamu haitakuwa kazi rahisi.

# TAMBWE: SIMBA SC ILISTAHILI UBINGWA

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa zamani wa Simba na Yanga, Amissi Tambwe, amesema kuwa Wekundu wa Msimbazi walistahili kutwaa ubingwa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu kutokana na ubora waliokuwa nao.

Tambwe ambaye aliichezea Simba msimu wa 2013/14 na kujiunga na Yanga msimu uliofuata hadi alipoachwa misimu miwili iliyopita, alisema kuwa Simba ilikuwa na wachezaji wenye uwezo mkubwa na kujituma, lakini ikiwa na wachezaji wabunifu kwenye eneo la kiungo ambao ndiyo wanaifanya sehemu ya nyuma na mbele kuonekana imara.

"Ni kweli soka la Tanzania lina figisu nyingi, lakini kwa hili, Simba walistahili ubingwa kutokana na kikosi chao jinsi kilivyokuwa, kilikuwa na wachezaji wazuri sana. Ukiwa na aina ile ya wachezaji kama wa Simba ni lazima utatwaa ubingwa tu," alisema Tambwe.

**Straika huyo alisema hata Yanga iliwahi kuwa imara wakati ilipokuwa na wachezaji akiwamo yeye na Simon Msuva, waliweza kupata matokeo mazuri na walikuwa hawakamatiki kirahisi.**

"Mimi (Tambwe), wenyewe na wengine tulitengeneza kikosi kizuri cha Yanga ambacho kilikuwa hakikamatiki, tulikuwa tunachukua ubingwa kwa sababu tulikuwa bora sana na wachezaji wetu walikuwa wakijituma sana," alisema Tambwe raia wa Burundi.

Straika huyo alisajiliwa na Simba msimu wa 2013/14 akitokea klabu ya Vital'O ya Burundi na akawa mfungaji bora kwa mabao 19, lakini msimu uliofuata akashika nafasi ya pili akiwa na magoli 14, moja akilifunga akiwa Simba na 13 akiwa Yanga, akijiunga na klabu hiyo baada ya kuachwa kipindi cha dirisha dogo la usajili msimu wa 2014/15, nyuma ya Simom Msuva aliyekuwa kinara kwa magoli yake 17.

Alitwaa kiatu cha dhahabu akiwa Yanga katika msimu wa 2015/16 akifunga jumla ya magoli 21, lakini hakuweza kutamba msimu wa 2016/17 ambao alipachika wavuni mabao 11, huku Msuva na Abdulrahman Mussa wakifungana kwa kila mmoja kufunga mabao 14.

USHABIKI...



Shabiki wa Polisi Tanzania (jina linahifadhiwa), akipiga picha ya 'selfie' na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Senzo Mbatha baada ya mechi ya Ligi Kuu Bara kati ya Maafande hao dhidi ya Wekundu wa Msimbazi kumalizika Jumapili iliyopita. Simba ilishinda mabao 2-1. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# Nne zafutiwa matokeo Zanzibar

**Na Hawa Abdallah**, ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limefuta matokeo ya mechi nne za Ligi Kuu Visiwani hapa kwa sababu ya kujihusisha na upangaji wa matokeo katika kipindi hiki cha kuelekea kumalizika kwa msimu wa 2019/20, imeelezwa.

Michezo hiyo ni kati ya Chuoni dhidi ya Mwenge, ambapo Chuoni ilipata ushindi wa mabao 3-0, Mafunzo dhidhi ya Jang'ombe Boys uliomalizika kwa sare ya mabaO 2-2, KMKM dhdi ya Jamhuri ambao baada ya filimbi ya mwisho kupigwa, KMKM ilishinda mabao 7-0 na Malindi dhidi ya Jamhuri.

Katika mchezo huo wa nne, Malindi walipata ushindi wa mabao 7-0 na michezo yote ilichezwa kwenye viwanja vya Mau.

Katibu wa Kamati ya Mashindano ya ZFF, Hussein Ahmada Vuai, alisema katika taarifa yake kuwa shirikisho hilo limechukua hatua hiyo baada ya kupitia ripoti ya waamuzi na wasimamizi wa michezo hiyo na kujiridhisha timu hizo zilijihusisha na upangaji wa matokeo.

Vuai alisema kila timu imetozwa fainali ya Sh. milioni moja kwa kila mechi iliyoshiriki kati ya michezo hiyo minne.

"Mchezo wa KMKM dhidi ya Jamhuri huo umefutwa na Jamhuri imepigwa faini ya Sh. milioni moja kwa kujihusisha moja kwa moja na upangaji huo wa matokeo," alisema Vuai.

Alieleza ZFF imetoa adhabu hizo kwa mujibu wa Kanuni ya Mashindano ya 22 (7) ya mwaka 2019-2020.

# Michezo

Alhamisi Julai 30, 2020
Nipashe




Beckham ajitosa kumsajili Suarez UKURASA 22



Mchezaji wa Chelsea, Reece James (kushoto), akijiandaa kumtoka beki wa kulia wa Wolves, David Coady katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa Jumapili iliyopita. Chelsea ilishinda mabao 2-0 na kukata tiketi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya. **PICHA: MTANDAO**

# PLUIJM AAHIDI MAZURI YANGA

## ●●● Awaambia mabosi wa klabu hiyo wasibahatishe, ajipanga kurejesha heshima...

**Na Somoe Ng'itu**

UAMUZI ni wao! Hayo ndio maneno ya aliyekuwa Kocha Mkuu wa Yanga, Mholanzi, Hans van der Pluijm, kuhusiana na tetesi za kurejea nchini kuchukua mikoba ya kuifundisha timu hiyo iliyoachwa na Luc Eymael.

**Pluijm ni mmoja wa makocha waliowahi kuiongoza Yanga kwa mafanikio, lakini aliondolewa na baadaye kwenda kufanya kazi Singida United ya Singida na Azam FC ya jijini Dar es Salaam.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Pluijm, alisema anasikitika kuona Yanga 'imepotea' tangu alipoondoka na endapo inataka kushinda mataji isifanye makosa katika kuchagua kocha mwingine atakayekiongoza kikosi cha timu yao.

Pluijm alisema anaifahamu vema timu hiyo pamoja na soka la Tanzania, hivyo kwake hatakuwa na wakati mgumu katika kutekeleza majukumu yake endapo atarejea nchini kufanya kazi.

"Ni juu yao, uamuzi ni wao, wao ndio wanajua wanataka klabu yao iende wapi, wanatakiwa kuwa makini kama wanataka mataji, hakuna kubahatisha," alisema Pluijm.

Mholanzi huyo alisema Yanga inatakiwa kuanza mapema maandalizi ya msimu ujao kwa sababu muda uliobakia kuelekea msimu mpya ni mdogo kwa sababu ya matatizo ya corona yaliyotokea hivi karibuni.

"Mpira wa miguu unachezwa hadharani, hauhitaji majaribio au miujiza, ni lazima maandalizi sahihi yafanyike, ukifanya hivyo, utatarajia matokeo mazuri, usipofanya, usitarajie makombe, itakuwa ngumu," alisema kocha huyo.

Aliweka wazi kwa sasa yuko huru, hana timu na anafanya shughuli zake binafsi kwenye makazi yake nchini Ghana.

"Sina timu, niko huru, nimepata salamu za kutakiwa lakini si rasmi, kama tutazungumza na viongozi na kufikia makubaliano, nitakuwa tayari kuja tena Tanzania, maisha ya mpira ni ya kuzunguka, unaweza kwenda mbali au ukarudi kule ulikotoka, kikubwa ni kuweka alama nzuri kila unapofanya kazi," Pulijm alisema.

Mbali na Pluijm, kocha mwingine ambaye ameweka wazi yuko tayari kurejea kuifundisha Yanga ni Mkongomani Mwinyi Zahera ambaye alimwachia mikoba ya kuiongoza timu hiyo, Eymael.

Yanga ilitangaza kuachana na Eymael mapema wiki hii baada ya kocha huyo kutoa kauli za kibaguzi na hivyo klabu hiyo pamoja na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kutangaza itamshtaki kwenye Shirikisho la Mpira wa Miguu la Kimataifa (Fifa).

# Simba yafikiria kuweka rekodi

**Na Mwandishi Wetu**

ZIKIWA zimebakia siku tatu kuelekea mchezo wa fainali ya Kombe la FA dhidi ya Namungo FC ya Lindi, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, amesema anataka kuweka rekodi ya kuiongoza timu hiyo kutwaa mataji mawili ndani ya msimu mmoja.

Tayari Sven ameiongoza Simba kutwaa taji la Ligi Kuu Tanzania Bara wakati mapema mwanzoni, Wekundu wa Msimbazi ikiwa na Patrick Aussems, ilichukua Ngao ya Hisani kwa kuwafunga Azam FC.

Sven aliliambia gazeti hili kuwa anahitaji kupata ushindi na kutimiza malengo yake ya msimu huu, hivyo anakiandaa kikosi chake kucheza soka la kiwango cha juu.

Mbelgiji huyo alisema wachezaji wake wako katika hali nzuri licha ya changamoto ya baridi waliyokutana nayo jijini Mbeya ambapo timu hiyo imeweka kambi.

"Baada ya kufanikiwa kutetea ubingwa wa Ligi Kuu tukiwa na mechi sita mkononi, malengo yetu yalielekea kutwaa Kombe la FA, hiyo ndio rekodi tunayoitafuta, tumejipanga na tutapambana kuhakikisha tunaifunga Namungo hapo Jumapili," Sven alisema.

Alisema wanajiandaa kupambana na changamoto ya uwanja na ndiyo sababu ya kufikia uamuzi wa kuweka kambi Mbeya badala ya Dar es Salaam.

"Tunataka kwenda kuweka rekodi ya kuchukua mataji mawili ndani ya msimu mmoja, tayari tumechukua ubingwa wa Ligi Kuu, sasa akili, mawazo na kila kitu kinaitaizama fainali ya FA, tunaendelea vema na maandalizi ingawa hali ya hewa ni baridi sana, tunawaambia wavae nguo nzito kwenye mazoezi ili kuwakinga wasiumie," Sven aliongeza.

Kikosi cha Simba kiliweka kambi Mbeya tangu Jumatatu na kinatarajia kuelekea Sumbawanga Mjini kati ya leo jioni na kesho kwa ajili ya mchezo wa fainali utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Nelson Mandela mkoani Rukwa.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >